# Mjadala habarishi kuhusiana na uchimbaji mdogo wa madini Tanzania

## Mapitio ya kimkakati ya changamoto na ufumbuzi

Fitsum Weldegiorgis na Abbi Buxton

Hati ya majadiliano
Octoba 2017

**Masoko endelevu; Usimamizi wa rasilimali za asili**

*Maneno Muhimu:*
Uchimbaji madini, uchimbaji mdogo wa madini, Mjadala

iied

## Kuhusu Waandishi

Fitsum Weldegiorgis ni mtafiti mwandamizi wa IIED na Abbi Buxton ni mshirika wa IIED.

Barua pepe ya Mwandishi: fitsum.weldegiorgis@iied.org; abbi.buxton@iied.org

## Shukrani

Waandishi wangependa kuwashukuru wadau wa uchimbaji mdogo wa madini wa Tanzania ambao mawazo na ushauri wao yamebeba maudhui ya karatasi hii. Tungependa pia kumshukuru Lucy Lynus anayewakilisha HakiRasilimali ambaye alisaidia kuratibu mijadala ya kimkakati ambayo ndio msingi wa kilichomo katika karatasi hii. Tunapenda pia kuwashukuru wataalamu wa maudhui, Dr Willison Mutagwaba na Dr Rosemarie Mwaipopo, ambao waliwasilisha changamoto muhimu na kuwezesha majadiliano kwa pamoja. Shukrani pia zimuendee Dennis Allan Eliashifie ambaye alitoa usaidizi wa tafsiri ya maneno na uratibu.

## Imetolewa na kundi la IIED linalohusika uundwaji wa masoko endelevu

Kundi la IIED linalohusika na masoko endelevu linafanya kazi ili kuhakikisha kwamba masoko ya ndani na ya kimataifa yanakuwa ya haki na usawa na yanaweza kuwasaidia watu masikini kunufaika na kustawi. Utafiti wetu unalenga juu ya mifumo, miundo na sera zinazopelekea kuwa na uchumi endelevu na jumuishi. Nguvu zetu ni kutafuta ufumbuzi sahihi wa ndani kwa changamoto za kitaifa na kimataifa.

## Mashirika wenzi/mbia

Karatasi hii ya mjadala imejikita katika mijadala ya kina iliyofanywa kwa kushirikiana na HakiRasilimali ambayo ni jukwaa la asasi za kiraia zinazofanya kazi za kimkakati katika sekta ya uchimbaji wa madini, mafuta na gesi nchini Tanzania. HakiRasilimali wanahusika kuchapisha kile unacholipa (Publish What You Pay) na imejikita katika agenda mbalimbali za uwazi kimataifa.
Mawasiliano: Coordinator@Hakirasilimali.or.tz

**HakiMadini** ni waandaaji wa majadilianao ya kitaifa yanayoratibiwa na IIED kuhusiana na uchimbaji mdogo wa madini Tanzania. HakiMadini ni taasisi isiyo ya serikali (NGO) Tanzania, ambayo lengo lake ni kuimarisha uwezo wa wachimbaji wadogo wa madini wa ndani ya Tanzania pamoja na jamii kushiriki na kufaidika na utajirin wa madini, pamoja na kutetea na kukuza haki za msingi za binadamu.
Mawasiliano: Amani Mhinda, Mkurugenzi Mtendaji (amani.mhinda@hakimadini.org)

**MTL Consulting Company Limited** ni watafiti wa Majadiliano ya kitaifa ya IIED ndani ya nchi ya Tanzania. MTL ilianzishwa mwaka 1998 kwa lengo la kutoa huduma za ushauri elekezi katika sekta ya rasilimali za asili, hasa madini, mafuta na gesi.
Mawasiliano: Willison Mutagwaba, Mkurugenzu Mtendaji (wmutagwaba@mtlconsulting-tz.com).

Octoba 2017

Weldegiorgis, F na Buxton, A. 2017. *Mjadala habarishi kuhusiana na uchimbaji mdogo wa madini Tanzania: Mapitio ya kimkakati ya changamoto na ufumbuzi.* IIED Discussion Paper, IIED, London.

International Institute for Environment and Development
80-86 Gray's Inn Road, London WC1X 8NH, UK
Tel: +44 (0)20 3463 7399
Fax: +44 (0)20 3514 9055
www.iied.org

@iied
www.facebook.com/theIIED

Pakua machapisho zaidi kupitia: http://pubs.iied.org

IIED ni wahisani waliosajiliwanchini Uingereza, Namba ya uhisani. 800066 na pia Scotland, OSCR Usajili namba SC039864 na ni kampuni pia ya udhamini (Limited Company) iliyosajiliwa Uingereza na kupewa namba ya usajili 2188452.

Sekta ya madini Tanzania imeanza miongo kadhaa iliyopita, ikihusisha uchimbaji wa malighafi mbalimbali (ikijumuisha dhahabu, shaba, fedha, platinum, bati), Madini ya vito (ikijumuisha almasi, tanzanite, garnets, saphires, rubies, emeralds) na madini ya viwanda (ikijumuisha chokaa, jasi, kaolin, chumvi na mchanga). Kwa kipindi kirefu, uchimbaji mdogo wa madini umekuwa ukitoa fursa za ajira na kipato kwa watu wake masikini lakini mambo mbalimbali yamekuwa yakikwamisha sekta ya uchimbaji mdogo kuwa wenye faida na tija. Changamoto zenye kipaumbele zilizobainishwa katika ushiriki na utafiti wetu wa ndani ni pamoja na mazingira ya kibiashara yasiyo rafiki, ubaguzi wa kijinsia, mvutano na wachimbaji wakubwa pamoja na serikali, sera zisizokubaliana na ngumu kuhusiana na masuala ya ardhi na leseni pamoja na matumizi ya ardhi yanayopingana. Kupitia majadiliano yanayojikita katika utekelezaji wa hatua muhimu, watendaji mbalimbali hawana budi kubainisha hatua zenye kipaumbele na ugawanaji wa majukumu ya utekelezaji ndani ya muongozo wa mabadiliko hasi. Mjadala utahitajika kutatua maswali kadhaa muhimu ikiwani pamoja na: jinsi gani utungaji wa sera pamoja na utekelezaji vinaweza kufanyika kwa njia ya ushirikishwaji na kijinsia? Ni hatua gani maalumu na za kweli ambazo zinaweza kuundwa, wadau muhimu na wawajibikaji wanaoweza kubainishwa, ushirikiano wa ufanisi ulioandaliwa kufikia matokeo hasi? Na ni majukumu gani yanayofaa kwa kuzingatia mahusiano ya kuheshimiana na yenye manufaa katika sekta ya uchimbaji mdogo.

# Jedwali la yaliyomo


**Muhtasari** 4

**Utangulizi** 7

**1 Kukuza sekta ya uchimbaji mdogo – uchimbaji wenye tija na uliounganishwa na biashara** 8

Kubainisha changamoto 9

Kubainisha ufumbuzi 9

**2 Kusaidia ushiriki wa wanawake katika uchimbaji mdogo wa madini** 13

Kubainisha changamoto 14

Kubainisha ufumbuzi 14

**3 Kuboresha uhusiano wa shughuli za uchimbaji mdogo na matumizi mengine ya ardhi** 17

Kubainisha changamoto 18

Kubainisha ufumbuzi 18

**4 Muingiliano kati ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa – na jukumu la Serikali** 22

Kubainisha changamoto 23

Kubainisha ufumbuzi 23

**Jiunge na mjadala** 26

**Vifupisho** 27

**Masomo yanayohusiana** 28

**Kumbukumbu** 29

**Kiambatanisho 1: Orodha ya washiriki: Uchimbaji mdogo Tanzania – Mijadala ya kimaudhui** 30

**Kiambatanisho 2: Dodoso: Uchimbaji mdogo Tanzania , mijadala ya kimaudhui** 33




PreDialogueASM_DP Swahili.indd 3 02/11/2017 11:45

# Muhtasari

## Umuhimu wa utafiti na ushirikishwaji wa wadau kabla ya mjadala.

Mpango wa mjadala na vitendo wa IIED kuhusiana na uchimbaji mdogo wa madini unahabarishwa na rekodi ya ufuatiliaji wa kipindi cha miaka arobaini katika kuimarisha mageuzi ya mabadiliko ya sera katika sekta ya madini, misitu na sekta nyingine. Imeandaliwa kusaidia wadau wa kitaifa kutambua ufumbuzi unaochochea urasimishaji, ufumbuzi uliojikita katika msingi wa haki, uchimbaji mdogo wenye tija, jumuishi na sekta inayowajibika. Mpango huu unatoa jukwaa linalohitajika kwa wadau mbalimbali kushirikiana na ubadilishanaji wa maarifa kuchochea utawala bora, kusikika kwa sauti za wadau, na kuhakikisha upatikanaji wa ajira zenye staha kwenye sekta ya madini na shughuli nyingine za maisha ya kijijini kama vile kilimo Mpango huu unajitahidi kuhakikisha kwamba wadau wote wanashiriki, mchakato huu unamilikiwa na nchi husika na kwamba mjadala unazingatia ufumbuzi. Kwa njia hii, mjadala chini ya IIED unaweza kusaidia kuunganisha wachimbaji wadogo na vipaumbele vya kitaifa na ajenda za maendeleo endelevu.

Mjadala wenye mafanikiounatakiwa kutanguliwa na mchakato wa kushirikisha na kuwaandaa wadau kwa ajili ya mjadala utakaojikita katika vitendo. Katika hatua ya majadiliano ya awali, mpangilio wampango wa IIED huanza na mtazamo kamili wa sekta ya uchimbaji mdogo wa nchi husika, mfumo wa kijamii na kiuchumi na utawala uliopo.Tunafanya hivi kupitia njia mbili –Utafiti wa kuhabarisha mjadala na ushirikishaji endelevu wa wadau kwa kushirikiana na mtafiti wa ndani ya nchi pamoja na mkutanisha wadau kwa ajili ya mjadala (Convenor). Shughuli hizi mbili husaidia kukusanya ushahidi ambao utawasilishwa katika mjadala wa kitaifa kuhusiana na changaoto mbalimbali za sekta ya uchimbaji mdogo wa madini.Pia katika hatua hii, tunabainisha wadau mbalimbali kulingana na eneo husika la kimkakati na majukumu ya awali katika kusaidia kutengeneza muongozo wa mabadiliko ya sekta katika mjadala wa kitaifa.

Mazungumzo katika mijadala ya awali, hutoa jukwaa kwa wadau wa kila sekta kujadili na kutoa mitazamo yao mbalimbali juu ya changamoto zinazoikabili sekta ya uchimbaji mdogo. Ushirikishwaji wa wadau na utafiti unaweka msingi wa kutambua ufumbuzi unaoweza kutekelezwa, majukumu ya kila mdau ndani ya sekta husika ambayo yanaeleweka. Yote haya ni muhimu kusaidia mjadala ambao:-

- Unawakutanisha wadau mbalimbali katika majadiliano ya kujenga (yaliyojikita katika ufumbuzi na usawa)
- Unatambua vipaumbele muhimu na hatua zinazofuata ndani ya muongozo wa mabadiliko hasi katika sekta ya uchimbaji mdogo.
- Unawapatia wadau mbalimbali majukumu yanayoeleweka katika muongozo wa mabadiliko hasi

## Kwanini mjadala ni muhimu katika sekta ya uchimbaji mdogo kwa Tanzania?

Uchimbaji wa madini ni shughuli muhimu na inayokuwa kwa kasi nchini Tanzania ikiwa na jumla ya wachimbaji kati ya milioni 1-1.5 ambao wanajishughulisha moja kwa moja na shughuli za uchimbaji mdogo kote nchini. Wakati mipango muhimu ya sera za uchimbaji mdogo imeanzishwa, sekta hii bado inakabiliwa na mapungufu mbalimbali ya kisheria na sera, mpangilio mbaya wa taasisi na kukosekana kwa muunganiko katika ngazi mbalimbali za chini na juu za kiutawala, viwango visivyoendana na mahitaji, uchimbaji mbaya, na kukosekana kwa uwezekano wa kuwa na maendeleo endelevu.

Sekta hii ya uchimbaji mdogo inakabiliwa na changamoto kubwa. Maslahi mbalimbali ya serikali na wadau yanayojitokeza yanabainisha umuhimu wa kuiendeleza. Mjadala wenye kushirikisha wadau na uliojikita katika ufumbuzi wa changamoto unahitajika ili kuchunguza na kuielewa sekta ya uchimbaji mdogo wa madini na kuja na makubaliano yaliyojikita katika mabadiliko ya sera na utendaji.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 4 02/11/2017 11:45

Wakati wa mjadala kuhusiana na uchimbaji mdogo kwa Tanzania umeshawadia. Kupitia ushirikishaji wetu wa wadau kabla ya mjadala, wadau walionyesha shauku yao, msisimko, utayari, na nia ya kushirikiana katika kutambua na kutekeleza ufumbuzi wa baadhi ya changamoto muhimu. Maendeleo katika sekta ya uchimbaji mdogo Tanzania ni muhimu kwa:

- Kuongeza uwezo wa sekta ambayo imekuwa ikitoa ajira muhimu na uwezekano wa upatikanaji wa mapato ya juu miongoni mwa watu masikini moja kwa moja au kupitia njia mbalimbali,
- Kupunguza migogoro kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa, kuongeza uwezo na faida zitokanazo na rasilimali za Tanzania, na kuboresha athari chanya na kupunguza au kutokomeza athari hasi za kimazingira na kijamii katika sekta ya madini,
- Kukabiliana na matatizo yanayosababishwa na uchimbaji mbaya wa madini na kuonyesha mifano mingi ya uchimbaji mdogo mzuri na wenye tija

## Kwenda na mwongozo wa mageuzi/ mabadiliko chanya

IIED kwa ushirikiano na HakiRasilimali, iliendesha mfululizo wa majadiliano mwezi wa Septemba 2017. Wakati wa majadilianao haya, washiriki kutoka sekta ya uchimbaji mdogo walijadili changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili sekta ya uchimbaji mdogo wa madini kwa lengo la kupendekeza ufumbuzi. Majadiliano yalijumuisha: Jinsi ya kuchochea uchimbaji mdogo wenye tija na muunganiko wa biashara, jinsi ya kuunga mkono ushiriki wa wanawake katika uchimbaji mdogo wa madini,jinsi ya kuhakikisha uwiano wa uzalishaji wa uchimbaji mdogo wa madini na sekta nyingine kama kilimo na matumizi mengine ya ardhi, kuboresha utegemezi miongoni mwa sekta hasa katika mtaji na nguvu kazi na jinsi ya kukabiliana na mvutano kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa. Washiriki walikuwa na kazi ya kutambua aina mbalimbali za ufumbuzi wa changamoto. Taarifa hii inawasilisha matokeo ya majadiliano hayo na orodha ya muda mrefu ya mageuzi makubwa na madogo yanayohitajika ili kuendeleza sekta ya uchimbaji mdogo wa madini kwa Tanzania na kuifanya iwe sekta inayowajibika na kuthibitishwa kuendesha maendeleo endelevu ya kiuchumi.

Pamoja na matokeo ya utafiti kwa ajili ya majadiliano ya uchimbaji mdogo wa madini kwa Tanzania na ushiriki wa wadau, matokeo ya majadiliano haya yanapaswa kuhabarisha mjadala wa utekelezaji kwa kusaidia kuunda muongozo wa mageuzi ya sekta ya uchimbaji mdogo wa madini Tanzania. Hii inapaswa kuhusisha maono ya pamoja ya mageuzi miongoni mwa wadau mbalimbali na kutambua majukumu ya kila mdau katika kutekeleza hatua zinazofuata. Wakati wa mjadala, washiriki watachagua kikundi cha uongozi na kujifunza (Learning and Leadership Group) ambacho kitapewa majukumu ya kuendeleza hatua mbalimbali zinazofuata kwa kufuata muongozo wa mageuzi utakaokubalika.

Kuna uhitaji kwa watunga sera kuangalia kwa karibu zaidi sheria zilizopo ili kuhakikisha kuwa sheria hizi zinazingatia masuala ya jinsia na sheria haziingiliani na kusababisha mkanganyiko katika kufanya maamuzi (sababu ya kusababisha rushwa). Ili kwenda mbele, mchakato na sera za kufanya maamuzizinahitaji kuwa za ushirikishwaji zaidi ukijumuisha sauti za wadau mbalimbali hasa zile za wanawake

Kukabiliana na ubaguzi dhidi ya wanawake nchini Tanzania, ambao kwa mda mrefu umekandamiza majukumu yao katika maendeleo ya uchumi na jamii ni muhimu katika kuboresha maisha ndani ya sekta ya uchimbaji mdogo wa madini. Mabingwa mbalimbali katika sekta tofauti tofauti walibainishwa kama wadau muhimu katika kukuza uwezo wa kijinsia na ujumbe wa aina mbalimbali kama vile umuhimu wa kuongeza njia mbalimbali za upatikanaji wa kipato katika maeneo ya vijijini na kukuza uhusiano mzuri kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa. Kundi la uongozi na kujifunza linapaswa kuundwa na mabigwa hawa na kutafuta namna ya kukabiliana na matatizo na chuki ambazo zinajitokeza katika vyombo vya habari na maoni ya umma na kudhoofisha uaminifu na ushirikiano.

Kuna uhitaji wa kujenga uwezo na kuendeleza ujuzi katika sekta zote za umma na sekta binafsi. Kuna umuhimu pia wakuwapatia taarifa muhimu pamoja na elimu mamlaka za serikali za mitaa, juu ya changamoto, ufumbuzi pamoja na majukumu yao.Serikali za mitaa ndio zenye jukumu muhimu katika kuziba pengo kati ya serikali kuu na wananchi mitaani.

Serikali kuu ina jukumu kubwa la kukabiliana na changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya uchimbaji mdogo kuanzia utungaji wa sheria ili kuhakikisha uwezo unakuwepo na ufanisi katika utekelezaji katika ngazi za chini. Ushirikiano wa ufanisi katika idara za serikali na usaidizi kutoka katika mashirika ya kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali ni muhimu ili kuhakikisha mafanikio ya sekta ya uchimbaji mdogo wa madini.

Wachimbaji wadogo na wakubwa pia wanapaswa kuwajibika kutokana na shughuli zao na katika kutekeleza mtazamo wa pamoja juu ya sekta ya uchimbaji wa madini. Njiaya kujifunza mmoja mmoja, kukuza ufahamu na kubadilishana maarifa ni njia ya gharama nafuu katika kukuza sekta ya madini.

Masuala mbalimbali pamoja na maswali kadhaa, yanabainisha ufumbuzi uliobainishwa kupitia mijadala ya awali, ushiriki wa wadau pamoja na utafiti na yamejadiliwa hapa. Majibu ya maswali haya yanapaswa kusaidia kuhabarisha muongozo wa mageuzi:

- Ni hatua gani za muda mfupi, wa kati na wa muda mrefu zinahitajika ili kuhakikisha utungaji wa sera nzuri za sekta ya madini?



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 5 02/11/2017 11:45

- Utungaji wa sera unaweza kufanywa vipi kuwa wa ushirikishwaji ukijumuisha watu wa ngazi za chini, uhalisia na vipaumbele?
- Ni maeneo gani ya kipaumbele serikali inapaswa kuyashughulikia? Je! Hii inafananaje na vipaumbele vya maendeleo ya kitaifa na mipango ya matumizi?
- Nini kinahitajika ili kusaidia wote na kuendeleza hatua mbalimbali ndani ya wizara ya madini, ofisi za madini za kanda pamoja na ofisi za madini za mkoa, nani ni watekelezaji muhimu au wadau muhimu katika ufumbuzi mbalimbali unaohitajika kwa sekta ya uchimbaji mdogo wa madini?
- Ni watu gani binafsi katika makundi yote ya wadau wanaoweza kuwa mabigwa/viongozi wazuri kwa ajili ya mageuzi katika maeneo muhimu kama vile uwezeshaji wa wanawake na ushikishanaji katika kufanya maamuzi.
- Jinsi gani ya kutoa nafasi kwa muendelezo wa mjadala na ushiriki miongoni mwa makundi ya wadau?
- Tunawezaje kuhakikisha sera nzuri zinafuatiwa na utekelezaji mzuri na makubaliano ya wadau mbalimbali juu ya utekelezaji wa majukumu? Ni majukumu gani muhimu ya kujenga uhusiano wa pamoja wa heshima na wenye manufaa katika sekta?
- Tunawezaje kushughulukia kikamilifu jukumu la wanawake katika sekta na kuimarisha sauti zao katika kuanzisha sera zinazozingatia jinsia na vitendo? Nani ni mabigwa/viongozi katika sekta hii nan i jukumu gani wanaweza kutekeleza katika kutatua kuendelea kwa changamoto na vikwazo mbalimbali vya kijamii na kiutamaduni?
- Tunawezaje kupanua na kuboresha kila kinachofanya vizuri katika mahusiano kati ya taasisi za umma na sekta binafsi?

## Hatua zifuatazo

Maswali ikiwa ni pamoja na yale yaliyotajwa hapo juu yalijadiliwa katika ushiriki wa awali wa wadau na mijadala ya awali na kupelekea kupendekezwa kwa ufumbuzi mbalimbali. Maeneo ambayo ufumbuzi mbalimbali ulipendekezwa yatawasilishwa na kujadiliwa pia katika mjadala wa kitaifa juu ya uchimbaji mdogo wa madini Tanzania ambao utafanyika mkoani Geita kati ya tarehe 7 na 10 Novemba 2017 na kuwakutanisha kwa pamoja wadau mbalimbali. Kupitia mchakato wa majadiliano, washiriki watakubaliana na vipaumbele na majukumu mbalimbali yatakayojadiliwa. Matokeo ya majadiliano yataandikwa na kusambazwa pia kwa wadau wengine wa kitaifa na kimataifa (na kupatikana pia kupitia www.iied.org) kama sehemu ya watu kufuatilia taarifa hii.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 6 02/11/2017 11:45

# Utangulizi

Mnamo Septemba 2017, IIED ilishirikiana na shirika la HakiRasilimali kuitisha majadiliano manne ya kimaudhui/ kimkakati juu ya uchimbaji mdogo Tanzania.Majadiliano haya ya kimkakati yanasaidia kushirikisha wadau katika majadiliano hai na kubainisha ufumbuzi yakinifu na unaotekelezeka kabla ya mjadala wa kitaifa. Mjadala wa kitaifa kuhusiana na uchimbaji mdogo Tanzania utafanyika mkoani Geita kuanzia tarehe 7 hadi 10 novemba 2017.Majadiliano ya awali kabla ya kufanyika kwa majadiliano ya kitaifa ni muhimu katika kuhakikisha kwamba mjadala wa kitaifa unakuwa mjadala unaolenga utekelezaji wa ufumbuzi na washiriki wanaandaliwa na kuwa tayari kwa ajili ya mjadala utakaokuwa unaangalia mbele zaidi na kujenga.

Kwa Tanzania, maudhui manne ya mijadala ya awali yalichaguliwa kulingana na maoni ya wadau mbalimbali katika kipindi tulipofanya kazi ya kutembelea Arusha na Dar es Salaam (Scoping visit) ambapo siku moja moja ilitumika kwa mikoa yote miwili mnamo mwezi wa septemba 2016. Maudhui/mkakati wa mjadala yalikuwa:

1. Wanawake katika uchimbaji mdogo (yalifanyika tarehe 5 September 2017 jijini Arusha)
2. Uhusiano wa uchimbaji mdogo na kilimo na matumizi mengine ya ardhi (yalifanyika tarehe 6 September 2017, jijini Arusha)
3. Biashara na uchimbaji mdogo:Fursa na changamoto kwa ukuaji wa shughuli za madini na biashara ( yalifanyika tarehe 11 September 2017, Jijini Mwanza)
4. Uhusiano wa uchimbaji mdogo na mkubwa na jukumu la serikali (yalifanyika tarehe 12 September 2017, jijini Mwanza).

Kwa ujumla, wadau 92 walishiriki katika mijadala ya kimaudhui. Hii ilijumuisha wachimbaji wadogo, watendaji katika mnyororo wa usambazaji na uongezaji thamani ikijumuisha wajasiriamali wa ndani wanaohusika kutoa huduma katika sekta, kama vile wachuuzi wa chakula na wasambazaji wa vifaa na wachakataji wa madini na wauzaji, viongozi wa serikali za mitaa na vijiji, wanachama na viongozi wa vyama vya wachimbaji wadogo vya mikoa na kitaifa, wawakilishi kutoka serikali kuu, mashirika ya kiaraia, vyombo vya habari, wasomi na wafadhili (angalia kiambatanisho 1 kwa orodha ya washiriki). Kufuatia uwasilishwaji wa changamoto muhimu za kimaudhui/kimkakati na majadiliano yaliyojikita katika ufumbuzi katika vikundi kazi (angalia kiambatanisho namba 2 kwa maswali yaliyotumiwa katika majadiliano), washiriki walibainisha orodha ya ufumbuzi unaowezekana kwa changamoto changamoto mbalimbali na wadau stahiki na ushirikiano stahiki unaohitajika ili kutekeleza ufumbuzi uliopendekezwa. Hati hii inashirikisha matokeo ya majadiliano hayo na inapaswa kuunda msingi wa majadiliano zaidi wakati wa mazungumzo ya kitaifa



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 7 02/11/2017 11:45

# Kukuza sekta ya uchimbaji mdogo – uchimbaji wenye tija na uliounganishwa na biashara

# 1

Sekta ya uchimbaji mdogo wa madini yeye tija na stahiki, na yenye athari chanya mbalimbali kibiashara, inahitaji upatikanaji wa masoko na fedha; wafanyakazi wenye mafunzo na wenye vifaa vya kiteknolojia na taarifa za kijiolojia; na mazingira ya uungwaji mkono na sera pamoja na na utekelezaji wake. Ingawa serikali ya Tanzania imepiga hatua mbele zaidi, kwa kutoa mazingira bora ya udhibiti na uendeshaji wa shughuli za uchimbaji mdogo, bado kuna mambo mengi yanakosekana. Kwa ufanisi wa sera na utekelezaji wa mafanikio, kuna haja ya: ushirikiano kati ya taasisi ndani na nje ya serikali; kubadilishana taarifa mara kwa mara na kwa njia ya uwazi(taarifa za leseni na sera za ardhi, taarifa za kijiolojia na bei za madini); kuboresha ujuzi juu ya uhalisia wa shughuli za uchimbaji mdogo(ikiwa ni pamoja na mahusiano ya jinsia); na uhamasishaji wa uchimbaji wa madini na biashara zote zinazohusiana na shughuli za uchimbaji wa madini. Wachimbaji wadogo wanahitaji kuwa thabiti katika kupata misaada na katika kukidhi matakwa ya sheria.

## Kubainisha changamoto

Wachimbaji wadogo wa madini wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ndani ya mazingira ya udhibiti na uendeshaji nchini Tanzania. Wachimbaji mara nyingi wanapata ugumu katika upatikanaji wa masoko, fedha na uwekezaji, mafunzo duni, vifaa na taarifa na kufanya shughuli katika mazingira magumu ya kiutawala. Kwasababu ya urahisi wa watu kujiingiza katika sekta hii, ambapo wachimbaji wengi wanashiriki uchimbaji wakitumia vifaa na maarifa ya kawaida, uchimbaji mdogo umekuwa ukitoa chanzo cha mapato na maisha kwa watu zaidi ya milioni nchini Tanzania, na zaidi ya milioni tatu hufaidika kutokana na uwepo wa shughuli za uchimbaji mdogo. Lakini changamoto hizi za muda mrefu, zinawazuia kuzalisha kwa kiwango kikubwa na kupata faida kubwa. Kukabiliana na changamoto za biashara zinakabiliwa na wachimbaji zitasaidia kutambua uwezo wa sekta na kuboresha maisha na mapato kwa mamilioni ya Watanzania.

## Kubainisha ufumbuzi

Washiriki walibainisha yafuatazo kama ufumbuzi muhimu kwa mafanikio ya uchimbaji wa madini na biashara zinazohusiana na shughuli za madini: upatikanaji wa mtaji; upatikanaji wa vifaa na ujuzi wa kijiolojia; ujuzi wa biashara na ujuzi wa kiufundi, kuhifadhi kumbukumbu vizuri; upatikanaji wa masoko na bei stahiki za madini; ushirikiano wa kisiasa wenye kujenga sekta ya uchimbaji mdogo; upatikanaji wa habari; na urasimishaji

Serikali ya Tanzania tayari imeenda mbele zaidi katika kutoa mazingira bora ya uendeshaji na udhibiti wa shughuli za uchimbaji mdoga:

- Sheria ya Madini ya mwaka 2010 inampa mamlaka Waziri wa Madini kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini. Hata hivyo, ukosefu wa kutofautisha wazi nani hasa ni wachimbaji wadogo imebainishwa kuleta changamoto mbalimbali. Katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2016/2017, waziri wa nishati na madini, alitangaza kuwa, baada ya tafiti za kijiolojia, maeneo 11 ya hekta 38,951 yametengwa kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini(MEM, 2016). Zaidi ya hayo, wakati wa majadiliano mshiriki kutoka Shirika la Madini ya Serikali (STAMICO) aliripoti kwamba maeneo 19 yaliyotolewa kwa wachimbaji wadogo yalikuwa katika hatua mbalimbali za utafiti wa kijiolojia.
- Mwaka 2015, serikali ilianzisha programu ya misaada ya kifedha kwa wachimbaji wadogo. Benki ya Maendelei Tanzania (TIB Development Bank) ilitoa dola milioni 3 kwa miradi 111 ya uchimbaji mdogo wa madini mwaka 2015/16, kulingana na Waziri wa Nishati na Madini katika hotuba ya Mei 2016 (MEM, 2016). Katika hotuba yake Waziri pia alisema kuwa karibu dola milioni 3.3 zilitengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo mwaka wa 2016/17 (ingawa fedha hizi zimechelewa kusubiri ukaguzi wa utoaji wa fedha katika awamu zilizopita).
- Serikali imerahisisha taratibu zake za utoaji wa leseni kwa njia ya ugawaji wa madaraka na kuanzisha mfumo wa kuomba leseni kwa njia ya mtandao ambao imepunguza gharama na mda pia unaotumika. Wachimbaji wengi wadogo kwa sasa wanaomba leseni zao kupitia simu zao za mkononi. Ukaguzi wa serikali ulipelekea leseni 2,153 (leseni 72 za utafutaji wa madini na leseni za uchimbaji mdogo wa madini ya 2,081) kufutwa kwani hazikutumika kwa matakwa yaliyokusudiwa (MEM, 2017). Hii ni muhimu kwani inahakikisha ardhi ya kutosha inakuwepo kwa waombaji wenye nia ya dhati.
- Kupitia sera yake ya maendeleo ya viwanda, serikali inatoa fursa zaidi kwa wachimbaji wadogo kuudha malighafi zao kwa wazalishaji wa viwanda Tanzania. Kwa kuimarisha uhusiano wa kibiashara, wanatengeneza fursa zaidi za kufadhili sekta ya uchimbaji mdogo na kwa namna nyingine mapato yatokanayo na uchimbaji mdogo yanafadhili biashara nyingine kama kilimo.

Ni muhimu kwamba sera hizi zinaundwa na kutekelezwa kwa ufanisi. Hii inahitaji mdhibiti mwenye mafunzo na ufanisi wa kuelewa hali halisi za mitaa/vijiji, kama vile jukumu la wanawake. Inahitaji ushirikiano kati ya taasisi mbalimbali (ndani na nje ya serikali) kutoa mafunzo na taarifa, na iwe rahisi kwa wachimbaji wadogo kuboresha shughuli zao na kuwa na faida. Pia ni muhimu kwamba taasisi hizi zinasaidia 'biashara zinazohusiana na madini' na hivyo kusaidia maendeleo ya kiuchumi ndani ya jamii

Washiriki wa uchimbaji mdogo wanahitaji kuwa thabiti katika kupata misaada inayopatikana na kutekeleza matakwa ya sheria ndani ya sekta.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 9 02/11/2017 11:45

Na mwishowe, kila mabadiliko yaliyopendekezwa hapa yanapaswa kuundwa na kutekelezwa kwa kuzingatia usawa wa jinsia ili kuongeza ufanisi katika sekta kwa ujumla.

## Upatikanaji wa fedha

Washiriki wa mjadala walibainisha upatikanaji wa mtaji kama moja ya kikwazo kikubwa kwa ukuaji wa biashara ya uchimbaji mdogo .

Ilibainishwa kuwa taasisi zisizo rasmi za fedha zinaweza kutoa huduma za haraka na rahisi za mikopo kwa wachimbaji wadogo. Wengi hawahitaji fomu za maombi, uhakikisho, dhamana au wadhamini na hivyo fedha zinaweza kupatikana mara moja. Kwa uhalisia, taasisi hizi zisizo rasmi ni chaguo pekee la kufadhili karibu na maeneo ya wachimbaji.

Lakini kwa sababu taasisi hizi za kifedha zinafanya kazi katika mfumo usio rasmi, taasisis hizi hazipo chini ya uangalizi na udhibiti na hazifungwi na sheria. Hii huchochea kuibuka kwa matatizo katika kudhibiti shughuli za uchimbaji mdogo na katika kulinda shughuli halali za uchimbaji mdogo kutokana na vitendo visivyokuwa vya haki.

Hivyo, ni suluhisho gani? Serikali ni mdau muhimu hapa. Shughuli zisizo rasmi za ukopeshaji, zinahitajika kufanywa kuwa rasmi. Serikali inahitaji kutambua na kurasimisha taasisi hizi za fedha kwa kutoa udhibiti ulio bora wa shughuli zao. Hii inahitaji mafunzo bora na taratibu za utekelezaji kwa watendaji wa serikali wanaofanya kazi ya kusimamia taasisi hizi.

Washiriki walisisitiza kuwa serikali haipaswi kulazimisha kodi kubwa kwa taasisi hizi za ukopeshaji, ambayo inaweza kuwaangamiza na kuwatoa nnje ya biashara. Badala yake wanapaswa kuhamasisha utendaji ulio bora na hivyo kuunga mkono maemazoea bora na kwa hiyo kuungndeleo ya shughuli za uchimbaji mdogo.

## Upatikanaji wa vifaa na utaalamu wa jiolojia

Upatikanaji wa teknolojia bora na inayofaa ni jambo lisilohitaji mjadala miongoni mwa wadau wa sekta ya uchimbaji mdogo; hasa aina ya teknolojia inayowawezesha wachimbaji kuelewa asili ya kijiolojia ya eneo hilo, pamoja na vifaa vya upatikanaji vinavyofaa kwa ajili ya uzalishaji na uzalishaji mazuri usio haribu mazingira. Hii inapaswa kusaidia juhudi za kuzuia matumizi ya kemikali hatari kama vile zebaki na cyanide.

MEM na Tume ya Madini ya Tanzania (TMC) wapo katika mchakato wa kuanzisha vituo vya ubora. Kuna msaada wa jumla kwa vituo hivi na mapendekezo kwamba, vituo hivi vitoe huduma za uchakatajiwa madini, mafunzo ya kiufundi na huduma za ugani, utafutaji wa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo, na taarifa za kijiolojia

Wadau wa uchimbaji mdogo wanapaswa kushirikishwa katika mchakato huu, ili kuhakikisha kuwa vituo hivi vimeundwa katika mfumo ambao ni jumuishi na shirikishi ili kutumikia madhumuni mbalimbali ya uanzishwaji wake: uchakataji, biashara, mafunzo na vituo vya usambazaji wa taarifa.

Ndani ya vituo hivi, STAMICO na TMC inapaswa kuwekeza katika utafiti wa madini katika maeneo ya wachimbaji wadogo. Taarifa za kijiolojia zilizokusanywa kupitia uchunguzi zinapaswa kuwekwa wazi kwa wachimbaji wadogo kabla ya kuanza shughuli zao za uchimbaji madini katika maeneo hayo..

Serikali inapaswa kufadhili wanajiolojia katika ngazi za chini - kwa mfano, huduma za ugani - kutoa tafsiri sahihi na ya wakati wa taarifa za kijiolojia

Wakati huo huo, washiriki wa uchimbaji mdogo wa madini na RMO wanapaswa kuungwa mkono kwa njia ya mafunzo na rasilimali ambazo zinaweza kutolewa na STAMICO, Chuo cha Uhandisi na Teknolojia, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA), Taasisi ya rasilimali za madini(MRI) na vyama vya wachimbaji wa madini vyamikoa (REMAs). Hii itasaidia washiriki wa uchimbaji mdogo kuwa wahusika zaidi katika kuzipata na kuelewa taarifa za kijiolojia kutoka STAMICO na GST, na kuboresha ufanisi zaidi.

## Maarifa ya biashara na ujuzi wa kiufundi

Mda na tena washiriki wa mjadala walionyesha kuwa ujuzi bora na ujuzi katika uchakataji na uongezajii thamani zinahitajika ili kuongeza umuhimu kwa soko la bidhaa zilizoongezwa thamani. Mifano ya ujuzi huu ni pamoja na kukata madin ya vito, kutengeneza na kusafisha.

Taasisi ya Rasilimali ya Madini inapaswa kuwa mdau muhimu katika kujenga uwezo wa kiufundi wa sekta ya uchimbaji mdogo wa madini.

Shiriko ya viwanda vidogo(SIDO) na VETA, kwa kushirikiana na REMAs na Tume ya madini Tanzania, zinaweza kusaidia biashara mpya kwa kutoa ujuzi na mafunzo ya kiufundi kwa njia ya programu za biashara

## Kuhifadhi kumbukumbu

Ili kuhusisha taasisi za kifedha na wawekezaji, wachimbaji wadogo wanahitaji kuandika na kuwasilisha taarifa muhimu kwa mfano, nani anamiliki nyenzo kuu za uzalishaji mali, ni kiasi gani wanachozalisha, ni kiasi gani wanaweza kuzalisha, na kwa muda gani.

Mashirika ya wachimbaji wadogo, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ,mashirika ya biashara ya jamii (CBOs) na asasi za kiraia yanapaswa kutoa huduma za msingi kwa washiriki wa uchimbaji mdogo katika kuhifadhi kumbukumbu.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 10 02/11/2017 11:45

Wakati huo huo, washiriki wa uchimbaji mdogo wanapaswa kutambua umuhimu wa kuhifadhi kumbukumbu kwa ukuaji wa biashara zao na, pale wapatapo nafasi waweke katika kujifunza.

## Upatikanaji wa soko na bei stahiki za madini

Wengi wa wachimbaji wadogo, huuza malighafi zao kwa wafanyabiashara wanaopatikana katika maeneo yao ambao nao wanafanya biashara zao katika njia zisizo rasmi. Wazalishaji mara chache sana wanapata bei stahiki kwa bidhaa zao. Udhibiti ni dhaifu na kuna uwazi kidogo kuhusiana na bei za madini.

Ili kukabiliana na hili, serikali inapaswa kutoa mwongozo juu ya bei za madini na vito. Benki ya Tanzania inaweza kuipatia Wizara ya madini bei za kila siku za madini kulingana na masoko ya kimataifa. Wizara ya madini inaweza kuwashirikisha wachimbaji wadogo taarifa hizi kupitia ubao wa matangazo katika ofisi zote za madini za mikoa na ubao wa matangazo katika ofisi za wilaya, mitaa na vijiji. Bei hizi elekezi zinapaswa kutumiwa na wafanybiashara na pia kujulikana na wachimbaji

Vituo vya ununuzi na vituo vya mnada vinaweza kusaidia kukuza thamani na upatikanaji wa masoko kwa kufanya kazi kama vituo vya uuzaji kwa watu ambao wanataka kufanya biashara ya madini tofauti. Vituo hivi vinaweza pia kuwa chanzo cha upatikanaji wa taarifa muhimu juu ya wingi, ubora na thamani ya madini yanayopatikana kwa muda fulani. Vituo vya kununuliwa kwenye maeneo ya mgodi vinaweza kutoa upatikanaji rahisi wa soko kwa kuhakikisha bei ya kuaminika, na kwa kukataa walanguzi, ambao wanaweza kuwanyonya wachimbaji.

Washiriki wa uchimbaji mdogo wanapaswa kushirikishwa katika kubuni na uendeshaji wa vituo hivi vya kununua na minada ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora.

Vyeti vya Fairtrade vinaweza kusaidia wazalishaji na waendeshaji kuunganishwa na masoko ya kimataifa, kuzalisha kwa ufanisi, na kupata zaidi kupitia kukidhi viwango vya Fairtrade na masoko ambayo hutoa bei nzuri na hivyo kuchochea maendeleo. Mfumo huu huwahamasisha wazalishaji kuzalisha na kuwekeza katika mfumo ambao unazingatia usalama wa mazingira na masuala ya kijamii.

Fairtrade Africa kwa kushirikiana na wadau kama Solidaridad, serikali za mikoa na REMAs zinahitaji kufanya kazi na watendaji mbalimbali katika sekta ya uchimbaji mdogo wa madini kuongeza ujuzi katika kuwatambua na faida zake wakati huo huo wakiendelea kujenga soko kwa bidhaa zilizokwisha thibitishwa.

Maonyesho maalum ya madini yanaweza kuonyesha kazi na bidhaa za wachimbaji wadogo, kukuza masoko. Matukio haya yanaweza pia kusaidia kutabiri muenekano mzuri wa sekta na kuhamasisha shughuli stahiki za uchimbaji mdogo wa madini.

MEM, STAMICO na TMC zinaweza kusaidia kuandaa vyama vya wachimbaji na wachimbaji wenyewe kujiandaa na kushiriki katika matukio haya. Matukio haya yanaweza kufanyika kwa msingi wa kila mwaka au kila baada ya nusu mwaka.

Bodi ya ushauri wa madini inaweza kusaidia kuboresha udhibiti na utekelezaji wake, hasa kwa madini ya vito kama zinnon, ruby, saphire na tanzanite, kwa kuunganisha pengo kati ya wachimbaji wadogo na watunga sera. Bodi hii ya ushauri inahitaji kuwa na wawakilishi kutoka kwa mashirika mbalimbali ya serikali, wachimbaji wadogo, wachimbaji wakubwa, na asasi za kiraia ili kusaidia kuhalalisha,kurasimisha na mchakato wa maendeleo ya biashara.

## Mhimili wa siasa uliohabarishwa vyema.

Upendeleo wa kisiasa na habari zisizo sahihi husababisha utata, matarajio yasiyo ya kweli na kushindwa kwa uwekezaji katika sekta ya uchimbaji mdogo. Hii imedhoofisha uwezo wa serikali kuendeleza na kukuza sekta ya uchimbaji mdogo kwa njia bora ya udhibiti na uwekezaji wa nje.

Tunawezaje kuhakikisha kuwa serikali inafahamishwa zaidi?

MEM na TMC wanapaswa kuunda timu ya kitaaluma ya kiufundi ili kushauri serikali kuhusiana na uchimbaji mdogo wa madini. Timu hii inapaswa kujumuisha watu binafsi wenye ujuzi wa uchimbaji mdogo katika madini ya aina mbalimbali, biashara ya madini, na ufadhili katika sekta ya madini; jiolojia, wanasheria na wanamazingira. Timu hii ni tofauti na bodi ya ushauri iliyotajwa mapema; ingeweza kukaa ndani ya wizara ya madini ili kuzalisha na kuhakikisha mtiririko sahihi wa taarifa, jumuishi na wa kina ili kuwahabarisha watunga sera.

## Sekta ya uchimbaji mdogo iliyorasimishwa

Kurasimisha shughuli za uchimbaji mdogo ni muhimu ili kuweza kukusanya kodi, kusimamia kwa ufanisi utoaji wa leseni za madini na matumizi ya ardhi yenye ushindani; kuhakikisha ulinzi na utunzaji wa mazingira; ustawi wa wafanyakazi; na kuhakikisha utaratibu wa usaidizi na uchimbaji wa madini ulio thabiti.

REMAs, na mihimili mingine kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na vyama vya wafanyakazi wanapaswa kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu jinsi ya kuzingatia kanuni za shughuli za uchimbaji mdogo wa madini. Wakati huo huo, wanapaswa kuelezea manufaa ya kurasimisha shughuli zao, kama vile upatikanaji wa mafunzo, vifaa, misaada na masoko



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 11 02/11/2017 11:45

Wachimbaji wadogo wanapaswa kuwa wahusika katika kurasimisha shughuli zao na kushiriki katika mafunzo yanayotolewa

## Biashara zinazohusiana na shughuli za madini

*"Wakati inaposemekana madini yamepatikana mahali,utashangaa kuona wachimbaji wadogo wengi na hata watu wengi zaidi wanahusika katika utoaji wa huduma nyingine. Utapata kuona wachuuzi wa chakula, salons za urembo na wengine wengi"(Mshiriki wa majadiliano)*

Uchimbaji madini unaweza kutoa mchango mkubwa katika kukua kwa uchumi wa ndani kwa kutoa fursa za biashara kwa wafanyabiashara wa ndani wa bidhaa na huduma. Kwa mfano, katika Jamhuri ya Afrika ya Kati kiasi cha dola milioni 144.7 zimeingia katika uchumi wa taifa kutokana na shughuli za uchimbaji mdogo wamadini(Benki ya Dunia, 2008). Nchini Mongolia, wastani wa milioni za kimarekani 505 hutumika kila mwaka katika shughuli za kiuchumi za ndani karibu na shughuli za uchimbaji wa madini(ibid).

Ili kuongeza uwezo wa sekta ya uchimbaji mdogo kuchochea ukuaji wa uchumi wa ndani, tunapaswa kwanza kutambua biashara zinazohusiana au kuunganishwa na shughuli za uchimbaji wa madini na mahitaji yao ya miundombinu. Pili, wamiliki wa biashara wanaweza kuhitaji mafunzo ya kuandika mipango ya biashara ili kupata fedha. Na mwisho , serikali na vyama vya wafanya biashara vinahitaji kusaidia kikamilifu maendeleo ya biashara na mashindano kupitia vikao vya kibiashara, maonyesho ya biashara, na kuendeleza ujuzi.

### 1. Kutambua biashara zinazohusiana/ unganishwa na shughuli za uchimbaji wa madini na mahitaji yao ya miundominu

Biashara zinazohusiana na shughuli za uchimbaji wa madini ni nyingi na zinatofautiana. Zinajumuisha biashara kuanzia watengenezaji wa vifaa ambao husafirisha bidhaa zao katika mikoa na kanda mpaka wachuuzi wa mitaani wanaouza chakula kwa wafanyakazi migodini. Ingawa kubainisha biashara hizi mbalimbali na uhusiano wake na shughuli za uchimbaji madini inaweza kuwa changamoto, taarifa hii inaweza saidia kuonyesha uwezo wa sekta ya madini kusaidia na kukuza uchumi wa ndani. Kukua huku kwa uwelewa wa sekta ya uchimbaji mdogo na faida zake itasaidia pia wanasiasa kupata imani na sekta ya uchimbaji mdogo wa madini.

Washiriki waliomba wizara ya madini kufanya utafiti ili kubainisha uhusiano kati ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini na biashara za ndani zinazotoa huduma na bidhaa katika sekta ya uchimbaji mdogo wa madini – pamoja na biashar nyingine zinazonufaika na shughuli za uchimbaji mdogo wa madini kama ilivyo katika sekta za kilimo na utalii. Ni muhimu sana utafiti huu ukizingatia usawa wa kijinsia kuhabarisha utungaji wa sera (Angalia kipengele namba 2 hapa chini)

Miundombinu mizuri na ya kuaminika - ikiwa ni pamoja na barabara, umeme na maji - ni muhimu kwa mafanikio ya shughuli za biasha

Wizara ya madini inapaswa kufanya kazi na wizara husika (ikiwa ni pamoja na Wizara ya Ujenzi, Usafiri na Mawasiliano, Mazingira, Nyumba na Makazi ya Binadamu, Maji na Umwagiliaji, Viwanda na Biashara) na mamlaka za serikali za mitaa (Halmashauri) kutathmini hali ya sasa ya miundombinu katika maeneo ya uchimbaji madini maeneo na kisha kutengeneza mpango wa uwekezaji na uboreshaji pale ambapo inahitajika

### 2. Kuanda mipango ya biashara

Mipango mizuri ya biashara iliyoandaliwa kwa mpangilio mzuri, inaweza kusaidia wamiliki wa biashara kupata fedha kupitia ruzuku au mikopo. Lakini wamiliki wa biashara wachache wanaelewa umuhimu wa mpango wa biashara au kuwa na ujuzi wa kuuandika.

Vyama vya wafanya biashara vinatakiwa kufanya kazi na taasisi za fedha na shule za biashara kama vile Chuo cha Elimu ya Biashara ili kuwafundisha wamiliki wa biashara kuandaa na kudumisha mpango sahihi wa biashara na kuonyesha pia faida zake.

### 3. Kuanzisha majukwaa ya biashara

Vikao vinavyowaleta viongozi wa wafanyabiashara pamoja vinaweza kukuza ushindani, ubunifu na biashara. Kujenga mitandao miongoni mwa wafanya biashara inaweza kukuza ushirikiano wa pamoja ambao husaidia kukuza uchumi na soko. Uboreshaji wa ubadilishanaji wa taarifa kupitia majukwaa ya biashara mbalimbali inaweza pia kuboresha upatikanaji wa bidhaa, huduma, mafunzo na fedha kwa waendeshaji wa biashara hizi.

STAMICO, Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi (NEEC) na wizara ya madini wanapaswa kushirikiana kuandaa majukwaa na vikao vya kuwakutanisha pamoja wamiliki wa biashara.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi (NEEC) linapaswa kuanzisha mafunzo maalumu kwa ajili ya biashara mbalimbali zinazofanyika katika maeneo ya uchimbaji madini kwa msaada wa wa mashirika yasiyo ya kiserikali na asasi za kiraia ambazo zimejikita katika mambo ya ujasiriamali na uwezeshaji wa kiuchumi.

Taasisi za fedha ikiwa ni pamoja na taasisi ndogo ndogo za kifedha , benki mbalimbali za ushirika na taasisi ndogo za kifedha (kama vile ushirika wa kuweka na kukopa na benki za jumuia za vijijini), zinapaswa kuwa na uelewa zaidi juu ya uwezekano wa uwepo wa soko na hatari zilizopo kwa biashara zinazofanya kazi katika maeneo ya uchimbaji madini.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 12 02/11/2017 11:45

# Kusaidia ushiriki wa wanawake katika uchimbaji mdogo wa madini

# 2



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 13 02/11/2017 11:45

Zaidi ya robo ya wachimbaji wadogo wa madini Tanzania ni wanawake (Dreschler, 2001). Lakini sehemu kubwa ya nguvu kazi hii ya uzalishaji mara kwa mara wanalipwa kidogo, hawathaminiwi na wanadhalilishwa. Ugumu katika kupata mikopo, soko imara na kutendewa haki, huzuia wanawake kuchangia kwa ufanisi katika uchumi na jamii. Ufumbuzi mwingi uliobainishwa katika sehemu ya 1 (Kuboresha mazingira mazuri ya biashara Tanzania) na sehemu ya 3 chini (Muingiliano wa shughuli za uchimbaji mdogo na matumizi mengine ya ardhi) imerudiwa hapa. Kwa kuzingatia usawa wa kijinsia, serikali inaweza kuongeza uwekezaji wake katika sekta ya uchimbaji mdogo wa madini na kusaidia kukabiliana na mifumo inayowazuia wanawake kuonyesha uwezo wao kamili. Mabingwa wa sekta katika usawa wa kijinsia, wenye ujuzi bora na maarifa sahihi, wanahitajika kuwa na jukumu muhimu la kubadilisha mitazamo ya kiutamaduni na kijamii juu ya wanawake.

# Kubainisha changamoto

Katika jamii za Tanzania, wanaume ndio wenye mamlaka ya kila kitu. Wanatawala kisiasa, mamlaka za maadili, upendeleo katika jamii na umiliki wa mali. Wanaume huzungumza badala ya wanawake na kufanya maamuzi katika famila, Wanaume wazee huamua mambo mbalimbali ya jamii.

Licha ya wanawake kushiriki katika kuchakata madini na kutoa huduma mbalimbali maeneo ya uchimbaji madini (Armah, na wengineo.,2016) hawaruhusiwi kumiliki ardhi na kufanya maamuzi ya kibiashara. Mambo haya ya uhalisia katika jamii huzuia wanawake kufaidika na ushiriki wao wa dhati katika shughuli za madini. Bila ya umiliki wa ardhi, wanawake hawawezi kutoa dhamana inayohitajika kwa ajili ya kupata fedha.

Unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji kutoka kwa wafanyabiashara ni jambo la kawaida na huzuia uwezo wa wanawake kupata masoko imara na pia bei nzuri kwa bidhaa zao. Ndani ya jamii, unyanyasaji wa kijinsia una athari mbaya kwa afya na usalama wa wanawake, watoto na wanaume wanaoishi katika maeneo hayo

Mjomba Hussein, anayejulikana kama 'Pili Hussein' (Mjomba Hussein), ni mwanamke maarufu wa Tanzania katika uchimbaji mdogo wa madini mjini Mirerani. Ingawa hivi karibuni alipata kutambuliwa kutokana na majukumu yake katika uchimbaji mdogo wa wanawake bado anaendelea kukabiliana na mambo ya ubaguzi.

*"Katika siku hizo nilihitaji kujifanya kama mwanaume ili kupata eneo la uchimbaji wa madini Mererani. Nilipitia, na bado ninakabiliana na udhalilishaji na ubaguzi. Lakini mimi sikupoteza matumaini, ingawa najua jamii ina mtazamo mbaya kwangu" (Mjomba Hussein)*

# Kubainisha ufumbuzi

Muongozo wa mageuzi ya sekta ya uchimbaji mdogo ambao ni wa kijinsia unahitaji kukabiliana na 1) Sheria zilizopo na sera zinazoiunda sekta pamoja na kanuni zake; na 2) mitazamo ya kijamii na kiutamaduni ambayo huzuia jamii kuwatambuwa wanawake na majukumu yao.

Mipango mingi iliyobainishwa katika sehemu ya 1, katika kukuza biashara za uchimbaji mdogo zenye faida na tija, na Sehemu ya 3, katika kuboresha muingiliano wa shughuli za uchimbaji mdogo na matumizi mengine ya ardhi, inahitaji kuundwa na kutekelezwa kwa namna ambayo inazingatia usawa wa kijinsia. Hii itasaidia watendaji kuongeza uwekezaji wao kwa kujumuisha idadi hii muhimu ya wachimbaji wadogo. Itasaidia pia kujumuisha masuala ya kijinsia katika utungaji wa sera na utekelezaji wake.

Wakati huo huo, serikali inapaswa kutekeleza sera zisizobagua wanawake ili kuwanufaisha wanawake. Sera hizi zinapaswa kuondoa vikwazo vinavyowazuia wanawake kupata ardhi, leseni za madini, fedha, taarifa za kijiolojia, mafunzo na zoezi la kufanya maamuzi.

Mwisho kabisa waliofanikiwa katika sekta hii wana jukumu muhimu la kuangalia masuala ya ubaguzi katika jamii ya Tanzania, kwa kuwawesha wanawake kikamilifu na kuonyesha mchango wao uliopo – katika jamii kisiasa, kiuchumi na kijamii.

## Mfumo wa kisheria na mageuzi ya taasisi

Ubaguzi dhidi ya wanawake umekita mizizi katika tamaduni za Tanzania na hivyo ni tatizo katika utungaji wa sera, utekelezaji wa sera, elimu na biashara. Majibu mapana katika sekta zote zikijumuisha taasisi za serikali na binafsi yanahitajika ili kutatua changamoto hizi. Marekebisho ya sera yanayozingatia usawa wa kijinsia hayana buni kutoa kipaumbele katika masuala ya umiliki wa ardhi na upatikanaji wa leseni za madini. Viongozi wa kisiasa, vyama vya wachimbaji wadogo na waelimishaji wanahitaji kupigania uwezeshwaji pamoja na haki sawa kwa wanawake

Vyama vya kitaifa vya wachimbaji wa madini wanawake (kama vile TAWOMA), chama cha wanawake wachimbaji wa madini Mererani na shirikisho la wachimbaji wadogo Tanzania (FEMATA) wanapaswa kushirikiana kikamilifu na watunga sera katika hatua za mwanzo za utungaji wa sera. Hili linahitaji kuanza na mapitio ya kijinsia ya sera tatu muhimu.

1. Sheria ya Ardhi ya Taifa Na. 5 ya mwaka 1999
2. Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.14 ya mwaka 1999
3. Sheria ya madini ya mwaka 2010.

Viongozi hawa wa sekta hizi wanapaswa kushirikiana na watunga sera na waandishi wa habari ili kuhimiza kupitia sheria na kukata utangulizi uliotolewa na sheria za kimila

Kamati za bunge, wizara ya madini na RMOs wana wajibu wa kufanya kama viongozi wa kuhakikisha fursa sawa kwa wanawake. Viongozi hawa wa kisiasa wanapaswa kuhamasisha kutokuwepo kwa ubaguzi kwa wanawake katika kupata mikopo ya kuanzia biashara zao na misaada, kuwezesha upatikanaji wa data za kijiolojia, kuanzisha programu mbalimbali za madini na kuhamasisha sheria zinazozingatia usawa wa jinsia.

Vyama vya wachimba madini vinapaswa pia kushirikiana na watoa elimu (elimu ya msingi, sekondari, elimu ya juu na ufundi) kufundisha na kuwahamasisha wanawake wa umri mdogo kufanya kazi katika sekta ya madini. Hii itasababisha ukuaji wa kizazi cha wanawake chenye nguvu, walioelimika na waliowezeshwa katika sekta ya madini.

## Upatikanaji wa huduma za kifedha

Serikali na taasisi za kifedha zinahitaji kutekeleza sera zisizo na ubaguzi ambazo zinaruhusu na kuwashawishi wanawake kupata fedha. Hii inaweza kumaanisha kupunguza kiwango cha michango ya kujisajili, viwango bora vya riba na masharti ya kulipa, na kutokuwepo kwa urasimu. Wizara ya madini na RMO zinaweza kusaidia kuanzisha mpango wa msaada wa kifedha kupitia benki za ushirika au taasisi ya kifedha iliyojikita katika sekta ya madini, sawa na zile zilizopo katika sekta ya kilimo, ambayo inaweza kusimamia misaada kwa wanawake.

Mageuzi kwa sheria ya umiliki wa ardhi na leseni ya madini itasaidia kwa kuwapa wanawake dhamana zinazohitajika kupata mikopo

## Upatikanaji wa masoko imara

Vituo vipya vya madini vinapaswa kusisitiza kuwa ni vya kijinsia na vinatambua vikwazo vya kijamii na kitamaduni wanavyokumbana navyo wanawake. Wanawake wanafaidika pale ambapo vituo vya madini vinaweza kutumiwa sio tu kwa kuongeza thamani, lakini pia kama kituo cha kuuza vitu na kama maktaba ya taarifa mbalimbali kuhusu madini. Mara nyingi shughuli za wanawake hujikita hujikita katika maeneo karibu na nyumba zao, hii huzuia fursa zao za soko na uwezo wa kupata habari. Kwa hivyo, vituo vya madini vinapaswa kuwa karibu na jamii za vijijini.

Halmashauri za Serikali za Mitaa/Vijiji, kwa msaada kutoka kwa serikali kuu, Wizara ya madini,RMO na Washirika wa maendeleo, wanapaswa kuunda na kuanzisha vituo vya madini katika njia inayozingatia usawa wa jinsia.

Watendaji binafsi na asasi za kiraia pia wanaweza kuwa na jukumu la kuhakikisha wanawake wanashiriki katika mipango na jitihada za kubadilishana taarifa.

## Fursa katika shughuli zinazohusiana na madini

Wanawake katika jamii za wachimbaji wa madini ni mara nyingi wanahusika katika kutoa huduma na bidhaa mbalimbali kwa wachimbaji. Hii inajumuisha uchuuzi wa chakula, kubeba ore kutoka sehemu moja hadi nyingine na kutengeneza vifaa vya uzalishaji vilivyotengenezw kwa njia ya asil. Wanawake wengine wanaendesha biashara hizi pamoja na migodi yao wenyewe.

Vidokezo vingi vya ufumbuzi vilivyobainishwa hapa vimeonyeshwa katika Sehemu ya 1 hapo juu. Ili kuongeza ufanisi, ufumbuzi huo unapaswa kuundwa na kutekelezwa katika njia ya usawa wa kijinsia.

Zoezi lililopendekezwa la wizara ya madini kubainisha biashara mbalimbali zinazohusiana na shughuli za madini,linapaswa kubainisha maeneo ya biashara ambazo wanawake wana uwezekano wa kushiriki na kufanikiwa. Wizara ya madini inapaswa kufanya kazi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, mashirika ya wanawake kama Shirika la wanawake la Umoja wa Mataifa (UN Women), Mtandao wa kijinsia wa Wanawake Tanzania (TGNP, Kituo cha Msaada wa kisheria kwa Wanawake, na vyama vya wachimbaji wa wanawake (kama TAWOMA) ili kupata wataalamu wa masuala ya jinsia.

Serikali kuu na serikali katika ngazi za chini zinapaswa kutekeleza sera na mipango inayowashawishi wanawake wamiliki wa biashara katika jamii za uchimbaji wa madini – Kupitia kutokuwa na ubaguzi katika sheria, fedha na upatikanaji wa masoko

Ushirikiano wa kugawana ujuzi kati ya NEEC na watoaji wa elimu unapaswa kukuza habari juu ya ujasiriamali, utofauti na uwekezaji katika wanawake. Wizara ya madini inaweza kusaidia kushirikiana na vyama vya wachimbaj ili kuwezesha kujifunza kutoka kwa wenzao walio katika hatua nyingine katika ngazi za kikanda au mkoa

Majadiliano na majukwaa mengi ya wadau katika ngazi ya kikanda na kitaifa itasaidia wafanya maamuzi kuelewa namna ya kuingiza masuala ya jinsia katika sekta. Vikao hivi vinapaswa kuhusisha wataalam wa kijinsia (kama vile Shirika la Wanawake wa Umoja wa Mataifa, TGNP na TAWOMA) pamoja na watetezi katika vyombo vya habari, elimu, biashara, mamlaka za serikali za mitaa na polisi ambao ni muhimu kwa kutetea na kuchochea mageuzi katika sekta hiyo

## Wanawake katika kufanya maamuzi

Tanzania imeshuhudia kuongezeka kwa wanawake katika nafasi za mamlaka zaidi ya miongo miwili iliyopita, na idadi kubwa ya wanawake wasomi na wabunge wanawake na mwanamke wa kwanza kuwa makamo wa raisi katika historia ya nchi. Hii imesababishwa na kuongezeka kwa ufahamu zaidi miongoni mwa wanawake juu ya uhitaji wa kujisimamia na kulinda haki

zao, sera za serikali ambazo zimesaidia ushiriki wa wanawake( Nafasi ya viti maalumu kwa wanawake katika bunge). Lakini mamo mengi zaidi yanaweza kufanyika ili kuimarisha jukumu la wanawake katika ufanyaji wa maamuzi.

Tume ya Madini ya Tanzania inapaswa kuhakikisha uwakilishi bora wa wanawake katika baraza katika ngazi ya kikanda na kitaifa. Hii inaweza kufanyika kwa msaada wa vyama vya wanawake vya kikanda na kimkoa.

Wachimaji wadogo wanawake na wafanyabiashara wanawake wanapaswa kuwa wahusika katika kujiweka mbele kwa nafasi za uongozi katika vyama vyao mbalimbali. Vyama hivi vinapaswa kujenga uwezo na ujuzi kwa viongozi wa kike (na wanaume) katika sekta hiyo ili kuwasaidia kuwa na ufanisi zaidi na endelevu

Kuna haja ya makundi ya wanawake-kama jumuiya za ushirika, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kijamii - kuandaliwa na kufanya kazi vizuri, na kwa makundi haya kuwa na nguvu. TAWOMA Inafaa kuwa na uwakilishi mzuri wa wachimbaji wa kike kutoka mikoa tofauti na uzoefu tofauti wa madini, ikiwa ni pamoja na wale wenye ujuzi wa madini ya dhahabu, madini ya vito na vifaa vya ujenzi. Hii itasaidia kukuza ushirikiano kati ya wanachama wake. Pia itaimarisha na kupanua mamlaka ya TAWOMA katika majadiliano ngazi za juu na ushawishi wa sera.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 16 02/11/2017 11:45

# Kuboresha uhusiano wa shughuli za uchimbaji mdogo na matumizi mengine ya ardhi

# 3



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 17 02/11/2017 11:45

Katika maeneo ya vijijini Tanzania, mara nyingi wachimbaji hufanya kazi kando na wakulima, wavuvi na wahifadhi. Watu wengi katika sekta tofauti hufanya kazi kwa msimu. Wakati shughuli za uchimbaji madini mara nyingi ni chanzo kikubwa cha mapato kwa kaya hizi za vijijini, inaweza kuwa na athari mbaya juu ya ardhi na watumiaji wake. Sheria zinazosimamia rasilimali za asili zinaweza kuingiliana na kuunda urasimu usiohitajika – chanzo za utokeaji wa mambo ya rushwa. Ni muhimu kwamba mipango jumuishi ya matumizi bora ya ardhi iandaliwe ili kupunguza migogoro na kuongeza matumizi endelevu na ya faida ya rasilimali za asili. Uandaaji wa mpango fanisi wa matumizi bora ya ardhi unahitaji kuwa wa ushirikishwaji, umoja, na unaoweza kubadilishwa kulingana na mabadiliko ya mazingira.ushirikiano wa kisekta na ubadilishanaji wa taarifa kwa njia ya uwazi ni muhimu kwa ufanisi katika kufanya maamuzi.

## Kubainisha changamoto

Shughuli za uchimbaji mdogo mara nyingi hufanyika kando na shughuli nyingine za maisha ya kila siku vijijini. Wakazi wengi wa vijijini wanafanya kazi kwa msimu, wakihama kutoka uchimbaji wa madini, kilimo,na shughuli nyingine za vijijini kila mwaka (Hilson, 2016). Ardhi inayotumiwa - au inayohitajika kwa matumizi na wachimbaji inaweza kuwa na mahitaji au matumizi na wakulima, wahifadhi,watu wa misitu na wavuvi. Bila umakini na ushirikiswhaji katika utungaji na utekelezaji wa sera, migogoro huibuka kutokana na watu kushindania ardhi, kazi na mali asili. Ushindani huu unaongezeka wakati watu wanaongezeka na kuna mahitaji makubwa zaidi ya ardhi. Na mara madini yanapomalizika, shughuli za madini zinaweza kuacha makovu makubwa na ya kudumu juu ya ardhi na wakazi wake.

Katika Tanzania, kama katika nchi nyingi, sheria zinazoongoza matumizi mbalimbali ya ardhi zinaingiliana mara nyingi. Kuna sheria ambazo zinatumika kwa sekta zote za ardhi kama Sheria ya Ardhi Na 5 (1999), Sheria ya Mipango ya Miji (2007), Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (2007) na Sheria ya Vijiji (1999). Na kisha kuna sheria za sekta maalum, ambazo zinatumika kinyume na sheria hizi za ardhi. Kwa wachimbaji, hii inajumuisha Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

*"Ukweli wa kuambiwa, mara nyingi kuna mkanganyiko katika utekelezaji wa sheria hizi na sera husika. Hali hii pia imeonekana linapokuja suala la kupata leseni ya madini na kufanya shughuli za madini. "(Mshiriki wa mjadala)*

Mbali na ardhi, mienendo ya kazi na uhamaji upo miongoni mwa sekta - hususan uchimbaji mdogo wa madini na kilimo – na kuathiri uzalishaji endelevu wa sekta. Zaidi ya hayo, kuna ukosefu wa mipango ya muda mrefu na uelewa wa umuhimu wa sekta husika, na kusababisha kushindwa kutumia fursa kutoka katika sekta yenye kuingiza kipato.

Sheria zinazokinzana na uwepo wa wafanya maamuzi mbalimbali, ni changamoto kwa wale wanaohusika na kutekeleza sheria, na huchochea uwepo wa rushwa. Kwa mfano, Sera ya Madini ya mwaka 2009 inahitaji mchimbaji mdogo wa madini kupata kibali cha uendeshaji wa shughuli zake kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kibali kutoka kwa mamlaka kama vile Wizara ya Rasilimali na Utalii. Bila ushirikiano wa ufanisi kati ya mamlaka hizi, mchakato huu huishia kuwepo kwa urasimu na maamuzi yenye mkanganyiko. Uwepo wa urasimu mwingi hupelekea kupoteza muda na fedha na inaweza kupekea rushwa na kudhoofisha ufanisi katika usimamizi.

Udhaifu katika ubadilishanaji wa taarifa miongoni mwa watendaji mbalimbali, huweza sababisha ufanyaji mbaya wa maamuzi na kuleta athari katika uzalishaji, jamii na mazingira. Hii ina athari hasi sio tu kwa uchimbaji mdogo ila pia kwa watendaji mbalimbali vijijini na miongoni mwa matumizi mbalimbali ya ardhi.

*"Kutokana na ukosefu wa habari, kuna hatari ya uvamizi na uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za uchimbaji mdogo au mkubwa. Hii ilitokea huko Chunya kwenye Mto Amani ambako wachimbaji wadogo walivamia kingo za mto waliposikia kuwa kuna dhahabu. "(Mshiriki wa mjadala)*

## Kubainisha ufumbuzi

Mipango ya maendeleo vijijini hufanikiwa vizuri zaidi pale ambapo imeanzishwa na kuundwa katika ngazi za chini (vijijini)na umiliki wa wazi wa jamii wa mipango ya muda mrefu.

Mpango wa matumizi bora ya ardhi unapaswa kutekelezwa na kumilikiwa na jamii, kuhakikisha kuwa imeundwa kwa ufanisi na endelevu kwa muda mrefu.

Inapaswa yenye uwezo wa kubadilika kulingana na mazingira - 'hati ya kufanya kazi' yenye uwezo wa kubadilika kuendana na mabadiliko ya serikali na vipaumbele vya maendeleo. Inapaswa kuchukua mtazamo wa muda mrefu na mfupi wa shughuli mbalimbali- kujumuisha uwekezaji, mazingira na mipango ya jamii pale ambapo shughuli za uchimbaji madini zitakuwa zinafanyika na pale shughuli za uchimbaji zitakapokuwa zimekamilika.

Mipango ya matumizi bora ya ardhi inapaswa kuzingatia habari mbalimbali kutoka kwa jamii na wataalamu (kama vile wanasayansi na wanasheria) juu ya matumizi ya ardhi

Utawala bora wa matumizi ya ardhi unahitaji ushirikiano mkubwa kati ya sekta na mihimili ya uongozi.

Ubadilishanaji bora wa habari na ufanyaji wa maamuzi kwa uwazi, utasaidia kukabiliana na rushwa katika ngazi zote za serikali

Ili kujenga mahusiano na kuwezesha ubadilishanaji wa habari katika sekta zote, mafunzo na maendeleo ya ujuzi yanapaswa kuchukua mbinu ya kuhusisha sekta zote husika - kutambua maeneo ambapo ujuzi na maarifa vinaweza kufundishwa

Kuna mifano ambapo shughuli za uchimbaji wa madini zinafanyika kwa ufanisi pamoja na shughuli za kilimo katika mikoa kama vile Geita na Tanga. Katikamaeneo haya, wachimbaji wadogo hutumia mapato yanayozalishwa kutoka sekta moja ili kuunga mkono sekta nyingine. Mererani, katika mkoa wa Manyara, wachimbaji wanawake wana mashamba madogo ya bustani za mboga ili kuzalisha chakula kwa familia zao na kuuza ziada inayopatikana. Mifano hii mizuri inapaswa kushirikishwa kwa wengine na kuungwa mkono katika sekta hiyo.

Madini ni sekta ya pili kubwa baada ya kilimo katika nchi nyingi za Afrika - Hutoa ajira halali na uzalishaji wa kipato muhimu. Ni muhimu kutambua mchango huu mzuri wakati huo huo kupunguza athari zake mbaya kwa jamii na mazingira

## Uwazi mkubwa na ushirikishanaji wa habari

Poor information sharing between government departments with different roles in land planning has led to contradictory decision making, bureaucracy and encroachment by some users onto land assigned to others. An underlying challenge is that important data, such as geological surveys and minerals studies, is not made public; or only made public through electronic means that are not accessible to all.

Ushirikishanaji wa habari duni kati ya idara za serikali na majukumu tofauti katika kupanga mipango ya matumizi ya ardhi, imesababisha ufanyaji wa maamuzi yenye mkanganyiko, urasimu na uvamizi wa baadhi ya watumiaji wa ardhi katika ardhi iliyotengwa kwa matumizi mengine ya tofauti. Changamoto ya msingi ni kwamba taarifa muhimu, kama tafiti za kijiolojia na tafiti za madini haziwekwi wazi kwa umma au zinawekwa wazi kupitia mifumo ya kielectroniki ambayo haipatikani na watu wote kwa urahisi.

Washiriki wa majadiliano walisisitiza kuwa na uwazi mkubwa na kushirikishana habari muhimu katika idara za serikali na wajibu wa kufanya maamuzi juu ya matumizi ya rasilimali za asili.

## Msaada wa kupanga matumizi bora ya ardhi

Mpango fanisi wa matumizi bora ya ardhi unapaswa kuhusisha ujuzi na maoni kutoka kwa vyanzo vingi - ikiwa ni pamoja na jamii (kuhakikisha wanawake wanahusishwa katika kubadilishana habari na katika kufanya maamuzi), serikali na 'wataalamu' (kama vile wanajiolijia na wanasheria). Inabidi iwe na uwezo wa kubadilika kulingana na vipaumbele vya maendeleo vya serikali. Aidha, mipango ya matumizi bora ya ardhi inapaswa kutambua mapungufu ambapo uwekezaji unahitajika katika huduma za jamii na utoaji wa huduma kwa jamii za madini

Halmashauri za Serikali za Mitaa na vijiji pamoja na idara husika za serikali zinatakiwa kutumia tathmini shirikishi za vijijini ili kuendeleza na kutekeleza vizuri mipango ya matumizi bora ya ardhi. Njia hii mara nyingi hutumiwa na mashirika ya kuchochea maendeleo endelevu na jumuishi katika mipango ya matumizi ya ardhi. Ni muhimu kukusanya pamoja ujuzi na maoni ya watu katika maeneo ya vijijini.

Kutokana na wanawake mara nyingi kutojumuishwa katika fursa za kupata ardhi ya kutosha kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo na kilimo, washiriki wa majadiliano walipendekeza kuwa Wizara ya Ardhi, Makazi na Maendeleo ya Miji na Ofisi ya Rais: Utawala wa Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhusika na kuhakikisha sera za kijinsia zinatekelezwa katika ngazi za mitaa/vijiji katika kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mbinu shirikishi zinaweza kusaidia maamuzi ya ushirikiano kati ya vitengo vya serikali vinavyohusika na kugawa ardhi na mipaka ya vijiji.

Wanasiasa wanapaswa kusaidia jamii kwa kutetea shughuli mbalimbali zinazozalisha kipato na kuhamasisha uwekezaji kulingana na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Hii inaweza kuanzishwa na kamati ya sekta chini ya TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Ardhi. Mamlaka za Serikali za Mitaa/vijiji zitakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera hizi.

## Sheria bora za matumizi bora ya ardhi

Washiriki walipendekeza kuwa sheria zinazosimamia madini na hifadhi za misitu zinahitajika kuunganishwa. Hii inaweza kusaidia kuweka mfano ni jinsi gani matumizi ya ardhi yaliyotafsiriwa yanapaswa kuheshimiwa, hasa pale yanaathiri maeneo ya hifadhi.

Baraza la Taifa la usimamizi na utunzaji wa mazingira, TMC, RMO na TAMISEMI zinapaswa kuhakikisha kuwa serikali la ngazi za chini zinashirikishwa kufahamu mipango ya usimamizi wa mazingira na kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa ufanisi.

Wanawake wanapaswa pia kuhimizwa na kuungwa mkono kushiriki katika kuendeleza sera na sheria ambazo zinasaidia umiliki wa ardhi. Mashirika ya wanawake, kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, idara ya haki ya kijinsia, madawati ya kijinsia katika ngazi za wilaya na madawati ya kijinsia katika vituo vya polisi, yanapaswa kutoa nafasi zaidi kwa wanawake kuwa na ardhi kama njia za uzalishaji.

## Kuwaleta juu/kuwinua walio chini

Sekta ya uchimbaji mdogo wa madini ni sekta ngumu yenye washiriki wanaotenda kazi zao katika mifumo mbalimbali, ujuzi, maarifa, na ufahamu. Maeneo wanapokimbilia wachimbaji wadogo wa dhahabu kutokana na kusikia tetesi za uwepo wa dhahabu (Gold rush), Wengi wa wachimbaji hawa hawana ujuzi mkubwa, wanachimba katika mfumo usio rasmi na wana ufahamu mdogo kuhusu athari za shughuli zao kwa jamii na mazingira. Hii inaleta utofauti na hudhoofisha wachimbaji wale wanaofanya kazi kwa bidii kufanya kazi kwa kufuata vigezo vya sheria, kufuata kanuni za mazingira na kijamii, na kuwa na mahusiano mazuri na jamii.

MEM, NEMC na TMC wanapaswa kutoa elimu ya uelewa kwa wachimbaji wadogo ambao hawajajisajili na kurasimisha shughuli zao za uchimbaji juu ya utunzaji wa mazingira na uwepo wa mahusiano mema na sekta nyingine. Hii itasaidia kuziba pengo kati ya washiriki katika sekta mbalimbali na kujenga mahusiano mema. Programu hizi za mafunzo pia zinaweza kutolewa kwa wachimbaji ambao walishajisajili au waliokwisharasimisha shughuli zao ili kuendelea kuwajengea uelewa na maarifa.

*"Hapo awali tulikuwa tunawaona wachimbaji wadogo wa madini kama maadui wa mazingira. Lakini sasa kuna utayari kutoka kwa wachimbaji wadogo kujifunza zaidi kuhusu utunzaji wa mazingira. "(Ofisa kutoka NEMC)*

## Ufumbuzi fanisi wa migogoro

Migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi kwa kiasi Fulani haiwezi epukika. Ajali mbalimbali zinaweza kutokea ambazo zina athari mbaya katika maisha ya kila siku. Kwa hiyo ni muhimu kuwa na mifumo iliyo ya uwazi ya ufumbuzi wa migogoro.

Mhimili wa mahakama na mamlaka za serikali za vijiji/mitaa zinapaswa kufanya kazi na Ofisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ili kuhakikisha kuwa migogoro imetatuliwa bila ya upendeleo wala rushwa.

## Sera za uwekezaji na upanuzi wa Uchumi

Serikali inapaswa kuchukua mtazamo wa muda mrefu na mtazamo mkubwa katika kusimamia akiba ya madini ya nchi.

Serikali inapaswa kuwekeza mapato yatokanayo na madini kwa maendeleo ya muda mrefu ya eneo hilo. Hii inapaswa kujumuisha uwekezaji katika shughuli zingine za maisha na miundombinu inayonufaisha sekta mbalimbali. Serikali haina budi kuhitaji ushirikiano kutoka idara mbalimbali ili kutambua maeneo ya uwekezaji wa muda mrefu. Hii inapaswa kuhusisha Wizara za Kilimo, Maji na Umwagiliaji, Nishati na Madini, Kazi, na Mamlaka za Serikali za Mitaa/vijiji. Uamuzi huu unapaswa kuwa wa ushirikishwaji na ukijumuisha maoni ya wadau husika katika ngazi za chini na mipango ya kijamii

Serikali inapaswa kutunga sheria kuruhusu Benki ya Tanzania kuhifadhi madini ya thamani kama vile dhahabu, almasi na tanzanite ili kuimarisha uwezo wake wa biashara katika masoko ya kimataifa.

Ukusanyaji wa mapato unapaswa kufanyika katika ngazi za chini ili kuhakikisha uangalizi bora na uelewa wa namna gani na wapi mapato ya madini yanapozalishwa.

*"Ukweli wa suala hili ni kwamba serikali bado inapoteza mapato mengi kutokana na biashara za ndani zisizotabuliwa ambazo hufanyika pale tu madini yanapotolewa ndani ya shimo" (Wachimbaji wadogo kutoka Geita)*

Serikali inapaswa kuimarisha uwezo na ujuzi wa ofisi za mapato kwa kuidhinisha serikali katika ngazi za chini kukusanya mapato katika ngazi za chini, Ofisi hizi zinapaswa kuwekwa karibu na maeneo ya madini na maafisa wanapaswa kuwa taarifa za kutosha na sahihi.

## Kuboresha ujuzi na teknolojia katika sekta zote

Kwa jamii za vijijini ili kufanikiwa ni muhimu kuendeleza ujuzi na teknolojia katika sekta na kwa watendaji. Mipango ya kuongeza thamani kwa bidhaa za ndani, ujasiriamali, usimamizi bora wa biashara, na kuboresha athari za kijamii na mazingira lazima ziwe jumuishi, na pale inapowezekana iwe ya kisekta ili kushirikishana maarifa, ujuzi na wajibu kwa maendeleo endelevu. Teknolojia na michakato mbalimbali inayotumiwa katika madini yanapaswa kuboreshwa ili kupunguza athari zao kwa shughuli nyingine za vijijini.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 20 02/11/2017 11:45

Programu za mafunzo zinazotolewa na waelimishaji na taasisi za kifedha juu ya ujuzi wa biashara na kuhifadhi kumbukumbu zilizoelezwa katika Sehemu ya 1 hapo juu, kwa mfano, zinapaswa kuwa zinapatikana kwa wakulima, wavuvi na watu wa misitu pamoja na wachimbaji. Washiriki/watendaji wote wanapaswa kufundishwa juu ya uendeshaji salama wa vifaa na mashine mbalimbali wanazotumia katika shughuli zao.

Halmashauri ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi ina mamlaka ya kuchochea programu ndogo ndogo za kiuchumi kupitia uwezeshaji wa kifedha kama vile Mwananchi Empowernment Fund, ambayo hutoa mikopo rahisi kwa vikundi. NEEC inapaswa kuhimizwa kutoa msaada zaidi kwa wachimbaji wadogo - kupata teknolojia kwa ajili ya shughuli za madini na kilimo, na kuhakikisha hili limefanywa kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Kwa hili kutokea, wachimbaji wadogo wanapaswa kujipanga vizuri na kujiandikisha katika vikundi kama ilivyo kwa benki za jamii za vijijini, na vikundi vya kuweka na kukopa.

MEM, Chamber of mines, waelimishaji (kama vile VETA, SIDO, na chuo cha uhandisi na Teknolojia) wanapaswa kufanya kazi kwa pamoja ili kuendeleza ujuzi wa wachimbaji wadogo katika kuchimba na kuchakata madini, kupunguza athari zake katika mazingira na kuboresha usalama kwa watu wanaofanya kazi katika sekta zote zilizo jirani. Wanaweza kutoa mafunzo ya kipindi kifupi karibu na maeneo ya madini au programu za mafunzo kwa wakufunzi.

Washiriki wa majadiliano pia walipendekeza kuwa asasi za kiraia na waelimishaji, kama vile Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, wanaweza kuwafundisha wachimbaji ambao pia wanafanya kazi kama wakulima kuunganisha kwa ufanisi shughuli zao kwa kutumia mbinu za kisasa za kilimo bora, maendeleo ya kilimo biashara na uongezaji wa thamani. Wizara ya Kilimo inaweza kuunga mkono mipango hii kwa kutoa pembejeo za kilimo na mikopo ya ruzuku kwa watu hawa.

Mwisho wachimbaji na wakulima wanapaswa kuwa na bima ili ziwasaidie wakati wa maafa ya asili au ajali. Vyama vya Mikoa vya wachimbaji wadogo kwa kushirikiana na vyama vya kitaifa kama FEMATA, TAWOMA na RMO, vinapaswa kuendesha vikao vya mafunzo kwa watoa huduma ya bima kutoka katika mashirika ya umma na binafsi kama vile Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa.

## Kutatua changamoto ya uhaba wa chakula

Shughili za uchimbaji madini zinaweza kuboresha usalama wa chakula kwa wafanyakazi na jamii ikiwa uhusiano uliopo kati ya madini na kilimo unaeleweka vizuri. Hii itahitaji wachimbaji kujua ardhi ambayo inafaa kwa kilimo na kutumia ardhi hiyo kwa kilimo au kuwekeza mahali pengine kwa ajili ya hifadhi ya chakula.

Maafisa wa ugani wa serikali ngazi za chini na mashirika ya serikali, kama vile Hifadhi ya Taifa ya Chakula na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, wanapaswa kuandaa semina za umma na mipango ya kuhamasisha wachimbaji kushiriki katika kilimo cha kati na kidogo.

Majukwaa ya kitaifa, kama vile 'maadhimisho 8-8' ya kila mwaka (ambayo huadhimishwa kila tarehe 8 Agosti katika Siku ya kitaifa ya wakulima ) yanaweza kutumika kama jukwaa la kuongeza ufahamu kuhusu ushirikiano mafanikio wa uchimbaji mdogo wa madini, kilimo na shughuli nyingine za vijijini,

Vyama vya wachimbaji madini vya mikoa na kanda vinapswa kuhimiza wachimbaji wadogo kuwekeza tena na kuongeza njia nyingine za upatikanaji wa mapato. Hili linaweza kufanyika pia kupitia siku ya wakulima kila mwaka – ambayo itakuwa ni fursa kwa wachimbaji wadogo kujifunza kuhusu misingi ya biashara ya mazao kilimo na kuhamasishwa kupanga mipango ya muda mrefu kuongeza au kutoongeza njia za upatikanaji wa kipato chao cha madini kupitia uwekezaji katika biashara ya kilimo.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 21 02/11/2017 11:45

# Muingiliano kati ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa – na jukumu la Serikali

# 4



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 22 02/11/2017 11:45

Mivutano katika shughuli za uchimbaji wa madini ya aina mbalimbali ipo pia Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine nyingi zenye madini.Mivutano hii hutokana na ushindani kwa rasiimali za madini, hata hivyo, mara nyingi husababishwa na kutokuaminiana kwa muda mrefu kulikosababishwa na mawasiliano duni na udhaifu katika usimamizi. Kukabiliana na mvutano huu kuna uhitaji wa kujenga uhusiano mpya wenye kuheshimiana, kuelewa, lengo moja na majukumu ya kila mmoja yaliyo wazi. Serikali ina jukumu muhimu la kuanzisha hatua kwa ajili ya kuboresha mahusiano kati ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa. Washiriki wote wanapaswa kushiriki katika jukwaa la majadiliano, ubadilishanaji wa taarifa na uwekezaji katika malengo yaliyo sawa. Hatua chanya na jumuishi, ni muhimu ili kuongeza mchango wa sekta katika maisha na maendeleo ya uchumi.

## Kubainisha changamoto

Muingiliano kati ya makampuni makubwa ya madini na wachimbaji wadogo una historia ndefu Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine zenye madini. Ushindani katika rasilimali za madini mara nyingi huleta wachimbaji wa viwango tofauti tofauti katika eneo moja.Shughuli za wachimbaji wakubwa na wadogo zinaongozwa na mihimili ya udhibiti sawa na sheria nyingi zinazotumika kwa wachimbaji wadogo hutumika pia kwa wachimbaji wakubwa. Pamoja na kushabihiana huku kwa sheria hizi za usimamizi, tofauti katika kiwango na uwezo mara nyingi muunganiko huu unakuwa muunganiko usio wa furaha.

Maeneo ambapo wachimbaji wakubwa na wadogo hufanya kazi kwa pamoja, mawasiliano duni yanaweza kusababisha migogoro. Wachimbaji wakubwa huwashutumu wachimbaji wadogo kuvamia ardhi yao, kuharibu mazingira na kutengeneza mazingira hatarishi ya usalama. Wachimbaji wadogo wanashutumu wachimbaji wakubwa kuchukua ardhi yao, kupendelewa na serikali na wanachafua njia za maji. Ufanisi na usanifu wa shughuli za uchimbaji mkubwa pamoja na mazingira bora ya mahali wanapoishi na kufanyia shughuli zao ni tofauti kabisa na jamii zinazozunguka eneo hilo ambapo wengi wao ni masikini na wanafanya shughuli zao za uchimbaji mdogo katika mazingira duni. Hii inaweza kusababisha hasira. Bila utaratibu bora wa kushughulikia malalamiko na majukwaa ya majadiliano mivutano hii husababisha migogoro.

Uchimbaji mdogo usio rasmi unatoa changamoto za ziada. Uchimbaji mdogo usio rasmi mara kwa mara huingilia maeneo ya wachimbaji wakubwa au kweny ardhi ya jamii – uvamizi huu unatokana na matarajio ya utajiri wa madini, na ufahamu mdogo kuhusiana na matakwa ya sheria ya madini. Wachimbaji hawa wasio rasmi sio wavamizi tu lakini mara nyingi husababisha uharibifu katika mazingira na jamii hasa pale inaposababisha migogoro ya jamii na kushindwa kufikia uchimbaji wa madini ulio thabiti. Kuhamishwa kwa kulazimishwa kunaweza sababisha vurugu na kutangaziana vibaya kwa pande zote za uchimbaji mdogo, mkubwa na serikali.

## Kubainisha ufumbuzi

Msingi wa kuimarisha uhusiano kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa na serikali unapaswa kujikita katika malengo ya pamoja, kuheshimiana, na majukumu yaliyokubalika na wadau wote.

Washiriki wote wanapaswa kufanya kazi pamoja ili kutambua maono ya pamoja katika sekta ambayo ni jumuishi katika uchimbaji wa madini wa viwango vyote. Hii inaweza kuungwa mkono kupitia programu ya kubadilishana ujuzi,shughuli za uhamasishaji na jukwaa la majadiliano. Mawasiliano yaliyo aminifu na ya wazi miongoni mwa washiriki wote yanapaswa kutambua kwa hakika uwezo na mapungufu ya washiriki wote na kusimamia matarajio kwa ufanisi. Mazungumzo ya upatanisho yanaweza kushughulikia malalamiko maalum ndani ya jamii na kupatanishwa na mashirika ya ndani pamoja na serikali.Vyombo vya habari pia vina jukumu muhimu la kuendeleza ujumbe wa mahusiano mazuri na ya usawa. Kutambua fursa za utekelezaji wa pamoja na muundo, inaweza saidia kujenga uhusiano miongoni mwa washiriki na kuvunja vikwazo vyote vilivyopo na vile vya kufikiri.

Watu binafsi, serikali, wachimbaji wakubwa na wadogo kila mmoja wana wajibu wa kuboresha sekta na jukumu lao ndani ya sekta. Kutambua majukumu ya kila mmoja na uwajibikaji katika sekta na kisha kutoa msaada na ushirikiano katika sekta hii ni ufunguo wa mafanikio.

### Majukumu ya Serikali

Washiriki wa majadiliano walibainisha majukumu kadhaa ambayo serikali inaweza kuyafanya ili kukuza uhusiano bora na ushirikiano kati ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa

Serikali inaweza kuwa mwenyeji wa 'semina za uhamasishaji' (mazungumzo ya umma) juu ya haki na majukumu ya uchimbaji mdogo wa madini. Hii inaweza kuhusisha umuhimu wa kufanya kazi kisheria, haja ya kuzingatia kanuni za kijamii na mazingira, matumizi ya ardhi sahihi chini ya Sheria ya Ardhi, na haja ya kuzingatia haki za binadamu na haki za wafanyakazi kwa mfano, ajira za watoto, na kadhalika. MEM, Wizara ya Ardhi na Makazi ya Binadamu, Mamlaka ya Usalama na Afya ya Kazini (OSHA) na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira wanapaswa kushiriki katika kutoa huduma hizi. Wanaweza kuungwa mkono na washirika wa maendeleo kama vile UNICEF, Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO), Jumuia ya wanasheria Tanzania, Proramu ya mazingira ya Umoja wa Mataifa (UN EnvironmentProgramme), na taasisi za kitaaluma na utafiti.

Serikali inaweza kuwa msuluhish katika migogoro kati ya wachimbaji wakubwa a wdogo. Katika hali ya mgogoro juu ya matumizi ya ardhi, serikali inapaswa kuangalia na kutoa ardhi maalumu kwa shughuli za uchimbaji mdogo yenye utajiri wa madini uliothibitishwa. Pale inapowezekana, Serikali inapaswa kuhimiza wachimbaji wakubwa kutoa baadhi ya maeneo yaliyo chini ya umiliki wao kisheria kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini kwa wachimbaji ambao wana uwezo wa kufanya shughuli zao za uchimbaji kwa kufuata kanuni na taratibu.

Wakati wa kutoa leseni za madini kwa wachimbaji wakubwa, mtiririko wa mawasilianao kati ya serikali kuu na serikali katika ngazi za chini ni muhimu. Wizara ya madini inapaswa kuwajulisha Mamlaka za Serikali za Mitaa/vijiji husika ambapo leseni za uchimbaji mkubwa zimetolewa. Hii itawawezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa/vijiji kutoa taarifa muhimu kwa jamii zinazoishi au kufanya kazi katika eneo hilo, kuandaa taratibu za hesabu na fidia, na kuweka utaratibu bora wa kushughulikia malalamiko.

Halmashauri za serikali za vijiji/mitaaa zinapaswa kuihabarisha wizara ya madini na wachimbaji wakubwa kuhusiana na aina ya shughuli mbalimbali na jamii zinazofanya shyghuli zao katika eneo hilo, hivyo wachimbaji wakubwa wanaweza kujiweka tayari na kuwajibika kwa ajili ya mahitaji yao.

Wizara ya madini inapaswa kuwa thabiti katika kushirikiana na mawaziri katika masuala ya kijamii na mazingira ili kuhakikisha leseni zinatolewa na wale wote waliopatiwa leseni wanapata ufahamu wa uhalisia wa mazingira na jamii pamoja na mipango yoyote ya maendeleo iliyopo katika jamii hiyo.

Watendaji wa kufanikisha haya yote kutokea ni wizara ya madini, mamlaka za serikali katika ngazi za chini, Ofisi za madini za mkazi (RMO), na GS. Wanaweza pia kuungwa mkono na REMAs na vyama vingine vya wachimbaji wa madini kama vile KIWATAMITA, FEMATA na TAWOMA.

Serikali pia inahitaji kuhakikisha mamlaka zake husika zinafanya kazi kwa ufanisi zikiwa na miundombinu stahiki na mafunzo, na bila ya rushwa. Hii inapaswa kujumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), polisi na mahakama.

## Majukumu ya mamlaka za serikali za mitaa/vijiji

Mamlaka za serikali za mitaa/vijiji zinachukua nafasi muhimu kati ya serikali kuu na kinachofanyika katika eneo husika. Mamlaka hizi za serkali zikijengewa uwezo wa ujuzi na maarifa ya kuwasiliana na wachimbaji wakubwa na wadogo, zinaweza kutekeleza jukumu kubwa la kuhakikisha mazingira mazuri ya utendaji kazi na kuishi.

Mamlaka za Serikali za Mitaa/Vijiji zinapaswa kuweka mifumo bora ya kuandikisha na kubainisha washiriki wa uchimbaji mdogo katika maeneo yao. Hii itawasaidia kufuatilia aina na maeneo ya uchimbaji mdogo na kuzuia uvamidhi wa ardhi ya wachimbaji wakubwa. Kazi hii yenye changamoto itahitaji uwekezaji na msaada kutoka kwa TMC, MEM na vyama mbalimbali vya wachimbaji

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuboresha uhusiano wao na ufahamu kuhusiana na uchimbaji mdogo kwa kufanya jitihada za kufikia na kushirikiana na sekta hii ya uchimbaji mdogo. Wanapaswa kutoa fursa kwa wachimbaji wadogo kuonyesha kazi zao na bidhaa zao, kwa mfano, kwenye maonyesho ya biashara ya Julai 7 na Maonyesho ya Siku ya wakulima kitaifa Agosti 8.

Serikali za mitaa/vijiji zinaweza kusaidia kukuza mawasiliano na uelewa kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo kwa kuandaa mashindano ya kijamii, maonyesho ya biashara ya ndani, bonanzas na matukio mengine ya kijamii. Matukio haya yanaweza kulenga changamoto maalum au fursa za kubadilishana maarifa.

Wizara ya madini, TAMISEMI na NGOs husika, zinapaswa kujenga uwezo wa Halmashauri za serikali za mitaa/vijiji kuingilia kati kwa niaba ya serikali kuu kuzuia au kuondokana na migogoro. Hii inapaswa kujumuisha kuboresha maarifa na taarifa sahihi juu ya majukumu stahiki ya wachimbaji wakubwa na wadogo, sheria husika, njia nzuri za utatuzi wa migogoro na mawasiliano mazuri. STAMICO, MRI na Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa Hombolo - Dodoma, miongoni mwa wengine, zinaweza kutoa msaada wa kiufundi na ushauri katika jitihada hizi.

## Majukumu ya wachimbaji wadogo

Wachimbaji wadogo wanapaswa kuwajibika na kuwa thabiti kufanya shughuli zao katika misingi ya kisheria na kuheshimu uongozi wa serikali na vyama vyao.

Wachimbaji wadogo wanahitaji kutambua jukumu lao kama watendaji wa mazingira na kulinda kikamilifu rasilimali za asili (kama vile wanyama wa mwitu, misitu, milima, njia za maji, maji na vitu vingine vya kipekee na muhimu vya ardhi). Programu za mafunzo, kundi kwa kundi zinaweza kusaidia kuongeza ufahamu juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira. Serikali za mitaa/vijiji na wizara ya madini wanaweza kufanya kazi na wachimbaji wadogo kufanya tathmini ya athari za mazingira, mipango ya utunzaji wa mazingira na mipango ya ukarabati wa ardhi. Mashirika mbalimbali yanaweza kusaidia wachimbaji wadogo na kuhakikisha wanafuata viwango vya kimataifa, ikiwa ni pamoja na NEMC, mkemia mkuu wa serikali, Programu ya mazingira ya Umoja wa Mataifa, Hakimadini na HakiRasilimali.

Wachimbaji wadogo wanapaswa kutambua uwajibikaji wao katika jamii na kurudisha sehemu ya mapato yao kwa jamii.Hii inaweza kuwa katika mfumo wa utoaji wa misaada ya upendo, au misaada kupitia kapu maalumu



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 24 02/11/2017 11:45

la fedha za misaada kwa kushirikiana na wachimbaji wakubwa ili kushughulikia vipaumbele mbalimbali ndani ya jamii.Inaweza pia kujumuisha kuboresha huduma za kijamii, miundombinu (kama vile ujenzi wa barabara na shule) au kutoa huduma za upatikanaji wa nishati kama umeme.

## Majukumu ya wachimbaji wakubwa

Licha ya utajiri mkubwa uliozalishwa kupitia shughuli za uchimbaji mkubwa, jamii zinazozunguka maeneo hayo ya uchimbaji bado zinaishi maisha ya kimasikini na miundombinu duni, usambazaji duni wa maji, elimu na huduma za afya. Hu ni mfano wa maeneo mengi kuzunguka Geita, Mererani na Nyamongo.

Uzoefu umeonyesha kuwa kufuata viwango vya kimataifa na kanuni stahiki zinaweza kusaidia kuongeza faida ndani ya eneo husika kutokana na uchimbaji mkubwa na kuimarisha ushirikiano mzuri kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa. Serikali inapaswa kuhakikisha kwamba viwango hivi na kanuni hizi zinawekwa katika mikataba ya madini

Michango ya wajibu kwa maendeleo ya huduma za kijamii (CSR) inaweza kusaidia kujenga uhusiano kati ya kampuni ya madini na jamii. Wachimbaji wakubwa wanapaswa kutekeleza mipango ya mafunzo ambayo hutoa msaada wa kiteknolojia na kiufundi kwa wachimbaji wadogo. Programu hizi zinaweza kuundwa pamoja na wawakilishi wa wachimbaji wadogo ili kutambua maeneo ya kubadilishana maarifa.

Mfano wa mafanikio wa hatua mbalimbali za ushirikiano katika miradi ya uchimbaji mdogo ni Rwamgasa ambao unahusisha mpango wa ushirikiano wa wadau mbalimbali kati ya serikali, Benki ya Dunia, Mgodi wa Dhahabu wa Geita, Kampuni ya madini ya Acacia, na FEMATA. Mradi sawa na huo, unapangwa pia kutekelezwa Tarime na Mgodi wa dhahabu wa North Mara. Miradi hii inaweza kutoa mifano ya mafanikio ambayo yanaweza kuigwa katika maeneo mengine na kuhamasisha makampuni mengine makubwa ya madini.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 25 02/11/2017 11:45

# Jiunge na mjadala

Kati ya tarehe 7 na 10 November 2017, IIED itaandaa Majadiliano ya kitaifa kwa ajili uchimbaji mdogo wa madini na washirika mbalimbali wa ndani kwa kushirikiana na HakiMadini kama muandaaji wa majadiliano na MTL Consulting kama mtafiti wa majadiliano haya ya kitaifa.

Kulingana na majadiliano katika mijadala ya kimaudhui na uchambuzi yakinifu uliowasilishwa hapa, washiriki katika Mjadala wa kitaifa watazingatia mfumo wa majadiliano yafuatayo katika kusonga mbele na muongozo wa marekebisho. Majadiliano yatatumia ufumbuzi muhimu uliopendekezwa kwa kila eneo la kipaumbele kama ilivyohabarishwa na utafiti uliokwishakufanyika, ushiriki wa wadau na mijadala ya kimaudhui. Lengo ni kuboresha ufumbuzi huu uliopendekezwa kwa ajenda za muongozo wa mageuzi. Wajibu na majukumu ya kila mdau yatabainishwa na kikundi cha kujifunza na uongozi kitachaguliwa kusimamia muongozo wa mabadiliko katika kipindi cha baada ya mjadala wa kitaifa.

Kitu muhimu kwa mafanikio ya majadiliano ni kwamba washiriki hawaishii kujadili tu bali wanabainisha orodha ya vipaumbele na majukumu ya wazi na wajibu wa kila mshiriki aliyehusika. Kwa njia hii, wadau wanaweza kukubaliana juu ya muongozo wa mageuzi hasi ya sekta.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MAENEO YA UFUMBUZI:** | 1. Sera na utekelezaji wa urasimishaji, amani na ushirikiano, upatikanaji wa ardhi na leseni.<br>2. Upatikanaji wa fedha<br>3. Upatikanaji wa teknolojia na vifaa; na ufumbuzi unaohusiana na afya ya mazingira na usalama<br>4. Upatikanaji wa masoko<br>5. 5.1. Kuboresha uchimbaji mdogo kuwa sekta yenye uzalishaji wenye tija.<br>5.2. Uhusiano wa uchimbaji mdogo na sekta nyingine na athari mbalimbali katika biashara | | | |
| **MALENGO** | | | | |
| **UFUMBUZI ULIOPENDEKEZWA (KABLA YA MJADALA)** | | | | |
| | Sera na kanuni | Ujuzi/utafiti | Ushiriki/ Mawasiliano | Mafunzo ya ujuzi |
| **UFUMBUZI UNAOWEZA KUTUMIKA (MJADALA)** | | | | |
| **WAJIBU WA WADAU (MJADALA)** | | | | |



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 26 02/11/2017 11:45

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ASM | artisanal and small-scale mining |
| CBO | community-based organisations |
| CSO | civil society organisation |
| CSR | corporate social responsibility |
| FEMATA | Federation of Miners' Associations Tanzania |
| LGA | local government authority |
| LLG | learning and leadership group |
| LSM | large-scale mining |
| MEM | Ministry of Energy and Mines |
| MRI | Tanzania Mineral Resources Institute |
| NEEC | National Economic Empowerment Council |
| NEMC | National Environment Management Council |
| NGO | non-governmental organisation |
| REMA | Regional mining association |
| RMO | Regional mining office |
| SIDO | Small Industries Development Organisation |
| STAMICO | State Mining Corporation |
| TAMISEMI | President's Office: Regional Administration and Local Government |
| TAWOMA | Tanzanian Women Miners' Association |
| TGWP | Tanzania Gender Networking Programme |
| TIB | Tanzania Investment Bank |
| TMC | Tanzania Mining Commission |
| VETA | Vocational and Education Training Authority |



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 27 02/11/2017 11:45

# Masomo yanayohusiana

Bass, S, Flores-Zavala, G and Weldegiorgis, F (2016) ASM dialogue programme: IIED scoping mission in Tanzania. http://pubs.iied.org/G04119/

Flores-Zavala, G (26 September 2017) Small ventures, big hopes(Stories of change in Tanzanian ASM) https://tinyurl.com/y7rrb8jc

IIED (2017) 'The time is right' for dialogue about sustainable ASM in Tanzania.www.iied.org/time-right-for-dialogue-about-sustainable-asm-tanzania

IIED (2015) Finding common ground: the human story of gold mining.http://pubs.iied.org/pdfs/16606IIED.pdf

IIED (2015)Kutafuta usawa kwa kila mtu: Hali ya ubinadamu kuhusu uchimbaji madini ya dhahabu. http://pubs.iied.org/16606KIIED/

IIED (2015) Gold mining: the search for common ground. https://social.shorthand.com/IIED/nCUEFHSXq/gold-mining-the-search-for-common-ground



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 28 02/11/2017 11:45

# Kumbukumbu

Armah, F A, Boamah, S A, Quansah, R, Obiri, S and Luginaah, I (2016) Working conditions of male and female artisanal and small-scale goldminers in Ghana: examining existing disparities. *The Extractive Industries and Society* 3(2) 464–474.

Dreschler, B (2001) Small-scale mining and sustainable development within the SADC region.IIED and WBCSD.https://pdfs.semanticscholar.org/d2a1/382d6f524da0c3e9ba142406c92dd33cf527.pdf

Hilson, G (2016) Farming, small-scale mining and rural livelihoods in sub-Saharan Africa: A critical overview. *Extractive Industries and Society3*(2) 547–563.

MEM (2017) Financial budgetary presentation.

MEM (2016) Budget Speech of the Minister of Energy and Minerals.19 May 2016.

World Bank (2008) Gender dimensions of artisanal and small-scale mining: a rapid assessment toolkit.http://siteresources.worldbank.org/INTOGMC/Resources/toolkit-web.pdf

# Kiambatanisho 1

## Orodha ya washiriki: Uchimbaji mdogo Tanzania – Mijadala ya kimaudhui

| JINA | TAASISI |
|---|---|
| 1. Wanawake katika uchimbaji mdogo | |
| William S. Wanga | Mtendaji wa kata |
| Emmanuel Mbise | HakiMadini |
| Roberty M. Songa | Mjasiriamali |
| Hawa Kiranga | KIWATAMITA |
| Joyce Ndaruku | HakiMadini |
| Rosemarie Mwaipopo | UDSM – Mtaalamu wa Maudhui |
| Eunice P. Negele | TAWOMA |
| Pili Husseni | Mchimbaji mdogo |
| Agripina Kasiani | Mchimbaji mdogo |
| Joram Wimmo | Action Aid Tanzania |
| Iman Hatib | Policy Forum |
| Blaise Burnier | SwissAid |
| George Mwafula | Baraza la uwezeshaji wa kiuchumi la taifa (NEEC) |
| Adam Kobelo | Chairman of the Mererani Township |
| Hamis Dafi | Mchimbaji mdogo |
| Mwanahamis Mzalendo | Mchimbaji mdogo |
| Mariam Hasan | Mchuuzi wa chakula |
| Martha Bitwale | Madini Cluster |
| 2. Muingiliano kati ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini na kilimo pamoja na matumizi mengine ya ardhi: Changamoto na ufumbuzi kwa maisha endelevu | |
| Frank Mkumbo | District Mineral Secretary |
| Leonard Manyesha | Mwenyekiti MBEREMA |
| William S. Wanga | Mtendaji wa kata |
| Charles Mershack | Tanzania Forest Conservation group (TFCG) |
| Emmanuel Mbise | HakiMadini |
| Msandae Ikusi Sambe | Mchimbaji mdogo |
| Roberty M. Songa | Mjasiriamali |
| Hawa Kiranga | KIWATAMITA |
| Joyce Ndaruku | HakiMadini |
| Neema Komba | TAWLAE |
| Rosemarie Mwaipopo | UDSM – Mtaalamu wa maudhui |
| Namsifuel Mahimbu | RECODA |
| Christopher Kadeo | GEREMA |



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 30 02/11/2017 11:45

| JINA | TAASISI |
|---|---|
| Curtius Msosa | MAREMA |
| Amatia A. Ngerera | TAREMA |
| Eunice P. Negele | TAWOMA |
| Eng David Mlabwa | MEM |
| Pili Husseni | Mchimbaji mdogo |
| Agripina Kasiani | Mchimbaji mdogo |
| Junior Mkuranya | Mjasiriamali |
| Joram Wimmo | Action Aid Tanzania |
| Iman Hatib | Policy Forum |
| Blaise Burnier | SwissAid |
| Angolile Rayson | PELUM – Tz |
| George Mwafula | Baraza la uwezeshaji kiuchumi la taifa (NEEC) |
| Adam Kobelo | Mwenekiti wa mji wa Mererani |
| Hamis Dafi | Mchimbaji mdogo |
| 3. Biashara kwa wachimbaji wadogo: Fursa na Changamoto kwa ukuaji wa biashara katika sekta ya madini na biashara nyingine zisizohusiana na madini | |
| Hawa Kiranga | KIWATAMITA |
| Martha Bitwale | Madini Cluster |
| Christopher Kadeo | GEREMA |
| Curtius Msosa | MAREMA |
| Erenest Sanka | MEM – Zonal mining officer |
| Ernest Wambura | Mjasiriamali |
| Fredrick Katundula | New Habari |
| Ali S. Ali | MEM – Zonal mining Officer |
| Tuna Bandoma | STAMICO |
| Golden Hainga | GEREMA |
| Wilson Mutagwaba | MTL Consulting Company Limited |
| Joseph Mangilima | Geita Gold Mining |
| Gonzaga Mungai | FAIRTRADE-AFRICA |
| Samwel Kalima | Mchimbaji mdogo |
| Mtalingi Hamzeh | Mchimbaji mdogo |
| Iman Hatib | Policy Forum |
| Eunice P. Negele | TAWOMA |
| Emmanuel Ngoyinde | SIDO |
| Augustino Kilugawa | AREMA |
| Majura Maingu | Ubunifu ASS |
| Ester J Nkware | Mchimbaji mdogo |
| Miriam James | Mchimbaji mdogo |
| Stefano Zablon | Mchimbaji mdogo |
| Joyce A Mlay | Madini Institute |
| Salum Mkango | Madini Institute |
| Prosper Rweyemamu | Tanzania Investment Bank |
| Joel Matatia | Rwamgasa Umoja SACCOS |



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 31 02/11/2017 11:45

| JINA | TAASISI |
|---|---|
| 4. Muingiliano wa wachimbaji wadogo na wakubwa pamoja na jukumu la serikali | |
| Hawa Kiranga | KIWATAMITA |
| Martha Bitwale | Madini Cluster |
| Christopher Kadeo | GEREMA |
| Curtius Msosa | MAREMA |
| Erenest Sanka | MEM – Zonal mining officer |
| Ernest Wambura | Mjasiriamali |
| Fredrick Katundula | New Habari |
| Ali S. Ali | MEM – Zonal mining Officer |
| Tuna Bandoma | STAMICO |
| Golden Hainga | GEREMA |
| Wilson Mutagwaba | MTL Consulting Company Limited |
| Joseph Mangilima | Geita Gold Mining |
| Gonzaga Mungai | FAIRTRADE-AFRICA |
| Samwel Kalima | Mchimbaji mdogo |
| Mtalingi Hamzeh | Mchimbaji mdogo |
| Iman Hatib | Policy Forum |
| Eunice P. Negele | TAWOMA |
| Emmanuel Ngoyinde | SIDO |
| Miriam James | Mchimbaji mdogo |
| Stefano Zablon | Mchimbaji mdogo |
| Joyce A Mlay | Madini Institute |
| Salum Mkango | Madini Institute |
| Prosper Rweyemamu | Tanzania Investment Bank |
| Joel Matatia | Rwamgasa Umoja SACCOS |
| Jozaka Bukuku | Baraza la uwezeshaji la Taifa |



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 32 02/11/2017 11:45

# Kiambatanisho 2

## Dodoso: Uchimbaji mdogo Tanzania , mijadala ya kimaudhui

### 1. Wanawake katika uchimbaji mdogo

**I.** Nini kifanyike kuwasaidia wanawake washiriki kwa usawa na kufaidika kutokana na shughuli za uchimbaji madini?

- Ni nini sheria, utamaduni, kijamii, elimu, kisiasa na fursa nyingine za kurekebisha maswala yasiyo sawa kijinsia?

**II.** Je, ni njia gani zinazoweza kutumiwa ili kuwawezesha wanawake kutoka kufanya kazi nzito hadi kuwa wamiliki na waendeshaji wa biashara za madini wenye mafanikio - katika hatua za uzalishaji na uchakataji wa mnyororo wa thamani?

- Sheria na sera za serikali na mifumo ya msaada
- Mifumo ya msaada ya taasisi zisizo za serikali

a. Mambo haya yanaweza kufanikiwa vipi? Zingatia taarifa za kijiolojia, upatikanaji wa mtaji, vifaa na masoko, ujuzi wa ujasiriamali na kanuni za motisha.

**III.** Ni fursa zipi na mifumo iliyopo kwa wanawake katika uchimbaji mdogo kukua katika mifumo yao ya upataji wa kipato

- Wachuuzi wa chakula, watoa huduma
- Mifumo mingine ya biashara Tanzania ambazo wanawake wanaweza kuiendesha kwa mafanikio

**IV.** Nini kinaweza kufanyika kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki katika kufanya maamuzi na kuanzisha taasisi imara kushawishi ufanyaji wa maamuzi?

- Ni jinsi gani wanatoa maoni yao na vipaumbele katika kufanya maamuzi?

### 2. Muingiliano wa uchimbaji mdogo na kilimo na matumizi mengine ya ardhi na changamoto pamoja na suluhisho kwa maisha endelevu

**I.** Nini kinatakiwa kufanyika ili kufaidika na shughuli za uchimbaji mdogo na shughuli za kilimo kidogo kusaidia maisha endelevu?

- Ni mambo gani ya kisheria, tamaduni, kijamii, kielimu, kisiasa, na fursa nyingine kutambua hili?

**II.** Kulingana na uhalisia wa madini kutojizalisha na wakati huo huo umuhimu wa kipato chake, ni fursa zipi zipo kusaidia kilimo kupanuka/kukua kutokana na fursa hizi?

- Sheria na sera za serikali na mifumo ya misaada
- Mifumo ya misaada ya taasisi zisizo za kiserikali

**III.** Je, Kuna mifano ambayo inaonyesha mafanikio ya matumizi ya faida ya uchimbaji mdogo kwa kilimo chenye faida au biashara zinazohusiana na kilimo ndani ya Tanzania na duniani?

- Ni sababu zipi za uwezeshaji? Sababu hizi zinaweza kufikiwa vipi? Mfano upatikanaji wa mtaji na masoko, ujuzi wa ujasiriamali, kanuni za motisha.

### 3. Biashara kwa uchimbaji mdogo: Fursa na changamoto za kukua kwa biashara za madini na zisizo za madini

**I.** Nini kifanyike kuwasaidia wachibaji wadogo kuanzisha, kuendesha na kukuza biashara za madini kwa mafanikio?

- Zingatia shera, tamaduni, jamii, elimu. Siasa na fursa nyingine kuwezesha hili.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 33 02/11/2017 11:45

**II.** Nini kifanyike kuwasaidia wachimbaji wadogo na washiriki wengine miongoni mwa jamii ya wachimbaji kuanzisha, kuendesha na kukuza biashara nyingine zisizo za madini zilizounganishwa na shughuli za madini kwa mafanikio?

**III.** Zingatia sheria, ufundi, siasa, jamii, elimu na fursa nyingine kuwezesha hili

**IV.** Ni namna gani sekta ya umma na binafsi zinaweza kusaidia wachimbaji wadogo kupata mitaji, na vifaa?

- Ni namna gani wafadhili na taasisi za fedha wanaweza kuvutiwa / kuhamasishwa kuwekeza katika sekta ya uchimbaji mdogo kwa njia ya mikopo na mifumo mingine?
- Je ni jukumu gani lililofanywa na wafadhili wa kifedha wasio rasmi (ufadhili na wafanya biashara, dealers na madalali) katika maendeleo ya uchimbaji mdogo?
- Nini faida ya ufadhili usio rasmi?
- What are the setbacks of informal financing?
- Ni namna gani ufadhili usio rasmi unaweza kuboreshwa ili kukidhi matakwa ya kisheria kufadhili shughuli za uchimbaji mdogo wa madini?

**V.** Ni namna gani sekta binafsi na ya umma wanaweza kusaidia wachimbaji wadogo kupata soko?

- Ni namna gani vyeti vya utambuzi na mipango mingine ya ushirikiano wa soko inaweza kusaidia biashara kwa wachimbaji wadogo?
- Nini kinahitajika kufanyika kutatua changamoto za upatikanaji wa cheti cha utambuzi na faida zitokanazo na kutambuliwa na Fairtrade?
- Ni namna gani watendaji katika mnyororo wa thamani wanaweza shirikiana katika kutatua masuala mbalimbali ya kijamii na kimazingira katika jamii za madini kuendeleza mnyororo wa wa usambazaji ulio wa haki na wenye kufuata maadili

## 4. Muingiliano wa uchimbaji mdogo na mkubwa na jukumu la serikali

**I.** Orodhesha jitihada maalumu/shughuli/programu na pendekeza ni namna gani zinaweza kutekelezwa kwa mafanikio kuharakisha amani na ushirikiano wa pamoja miongoni mwa wachimbaji wadogo na wakubwa.

**II.** Nini jukumu la serikali (kitaifa na katika ngazi za mkoa) katika kutatua mivutano na kukuza uwepo wa amani baina ya wachimbaji wadogo na wakubwa:

- Hatua za muda mfupi?
- ndani ya mifumo ya utawala kama urasimishaji wa shughuli za uchimbaji mdogo?

**III.** Je, nini ni jukumu la sasa la serikali za mitaa/vijiji / wilaya katika kuhakikisha uwepo wa amani kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa?

- Yapi ni majukumu ya ziada yanaweza kufanywa na kila ngazi ya serikali miongoni mwa ngazi mbili za serikali?

**IV.** Nini jukumu la wachimbaji wadogo na wakubwa? Sio tu katika kutambua uwepo wa amani kutokana na mitazamo yao ila pia kutengeneza mifumo ya ushirikiano?

- Jukumu la wachimbaji wakubwa:
- Jukumu la wachimbaji wadogo:

**V.** Nini kazi na athari za huduma za maendeleo ya kijamii (CSR) na codes za kimataifa, kanuni na jitihada za kujitolea za mashirika mbalimbali kwa uhusiano wa wachimbaji wadogo na wakubwa.



PreDialogueASM_DP Swahili.indd 34 02/11/2017 11:45

PreDialogueASM_DP Swahili.indd 35 02/11/2017 11:45

Sekta ya madini Tanzania imeanza miongo kadhaa iliyopita, ikihusisha uchimbaji wa malighafi mbalimbali (ikijumuisha dhahabu, shaba, fedha, platinum, bati), Madini ya vito (ikijumuisha almasi, tanzanite, garnets, saphires, rubies, emeralds) na madini ya viwanda (ikijumuisha chokaa, jasi, kaolin, chumvi na mchanga). Kwa kipindi kirefu, uchimbaji mdogo wa madini umekuwa ukitoa fursa za ajira na kipato kwa watu wake masikini lakini mambo mbalimbali yamekuwa yakikwamisha sekta ya uchimbaji mdogo kuwa wenye faida na tija. Changamoto zenye kipaumbele zilizobainishwa katika ushiriki na utafiti wetu wa ndani ni pamoja na mazingira ya kibiashara yasiyo rafiki, ubaguzi wa kijinsia, mvutano na wachimbaji wakubwa pamoja na serikali, sera zisizokubaliana na ngumu kuhusiana na masuala ya ardhi na leseni pamoja na matumizi ya ardhi yanayopingana. Kupitia majadiliano yanayojikita katika utekelezaji wa hatua muhimu, watendaji mbalimbali hawana budi kubainisha hatua zenye kipaumbele na ugawanaji wa majukumu ya utekelezaji ndani ya muongozo wa mabadiliko hasi. Mjadala utahitajika kutatua maswali kadhaa muhimu ikiwani pamoja na: jinsi gani utungaji wa sera pamoja na utekelezaji vinaweza kufanyika kwa njia ya ushirikishwaji na kijinsia? Ni hatua gani maalumu na za kweli ambazo zinaweza kuundwa, wadau muhimu na wawajibikaji wanaoweza kubainishwa, ushirikiano wa ufanisi ulioandaliwa kufikia matokeo hasi? Na ni majukumu gani yanayofaa kwa kuzingatia mahusiano ya kuheshimiana na yenye manufaa katika sekta ya uchimbaji mdogo.

IIED ni shirika linalojihusisha na mambo ya sera na utafiti. Tunachochea maendeleo endelevu ili kuboresha maisha na kulinda mazingira haya ambayo maisha ya kila siku yanategemea. Tumebobea katika kuunganisha vipaumbele vya ndani na changamoto za kimataifa. Makao makuu ya IIED yapo London na inafanya kazi katika nchi za Africa, Asia, Latin America, Mashariki ya kati na Pacific na watu waliopo katika hatari zaidi. Tunafanya kazi nao ili kuimarisha sauti zao katika majukwaa ya kufanya maamuzi yenye athari kwao – kuanzia katika mabaraza ya vijiji mpaka mikataba ya kimataifa.

iied

International Institute for Environment and Development
80-86 Gray's Inn Road, London WC1X 8NH, UK
Tel: +44 (0)20 3463 7399
Fax: +44 (0)20 3514 9055
www.iied.org

Knowledge Products

Funded by:

SWISSAID

IGF INTERGOVERNMENTAL FORUM on Mining, Minerals, Metals and Sustainable Development

THE TIFFANY & CO. FOUNDATION